

**KUCHUNGUZA MILA NA DESTURI ZA MWANAMKE WA VISIWANI
PAMOJA NA FANI KATIKA TENZI ZA HOWANI NA MWANA KUKUWA**

FATMA ALI MOHAMED

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2016

UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma Tasnifu hii iitwayo:

“Kutathmini Mila na Desturi za Mwanamke wa Visiwani katika Tenzi za Howani na Mwana Kukuwa” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzani kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Digrii ya Uzamili M.A. (Kiswahili – Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

Tarehe

HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile sehemu yoyote ya Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyengine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi **Fatma Ali Mohamed**, nathibitisha kwamba, hii ni kazi niliyoifanya mimi mwenyewe na kwamba haijawasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kingine kabla kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

Sahihi

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa mama yangu mpenzi Time Omar Hamad na mume wangu mpenzi Bedwy Nassor Mbarouk wanaoishi Kifumbikai Wete Pemba, kwa mioyo yao mikunjufu kwangu. Nawaombea kwa M/Mungu awajali afya njema yenye manufaa na awajalie khatma njema pindi atakapowahitaji.

Aidha kazi hii naitabaruku kwa watoto wangu wapenzi Ajlat na Adil kwa kuvumilia tabu na shida katika kipindi hiki nilichokuwa masomoni na hivyo kukosa kutekeleza kikamilifu majukumu yangu kwao kama mama. Namuomba M/Mungu awajalie makuzi mema.

SHUKRANI

Awali ya yote natoa shukrani zangu za pekee kwa M/Mungu muumba kwa kunijalia uzima na amani katika moyo kwa muda wote niliokuwa masomoni. Pili shukrani za dhati kabisa zimfikie msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kuniongoza vyema katika kazi hii, kwa sababu kazi hii isingepiga hatua yoyote wala kukamilika bila ya ushauri na usimamizi wake. Aliisoma kazi hii na kuirekebisha bila ya kuchelewa na kuniongoza kikamilifu. Profesa Baraka na neema za Mungu ziwe nawe siku zote za maisha yako.

Aidha nawashukuru wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao walinifunza au kunipa mawaidha ya kimasomo katika kipindi hiki nilichokuwa masomoni. Nao ni Profesa Sengo, Dokta Mohammed Omar, Dokta Peter Lipembe, bila kumsahau Mwalimu Bakar Kombo Bakar.

Shukrani nyengine ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya Uzamili. Bila ya kumsahau Mwalimu Ali Mussa Faki kwa maelekezo aliyonielekeza kwa lengo la kukamilisha utafiti huu.

Vilevile natoa shukrani kwa watoto wangu walezi Riziki Jadi na Farida Jadi kutokana na mioyo yao ya kujitolea kwa kuwalea wadogo zao katika kipindi chote cha masomo yangu, bila ya kumsahau Khadija Haji kwa kumlea mtoto wangu bila pingamizi. Shukrani nyengine zimwendee Mr. Fakihi Yussuf kutokana na ushauri wake nzuri ambao ulisaidia kuikamilisha kazi yangu. M/Mungu atawalipa kheri.

Mwisho, sitoweza kuwataja wote waliochangia kazi hii mmoja baada ya mwengine, lakini natoa shukrani za dhati kwa nyote mliochangia kwa njia moja au nyengine kwa kuifanikisha kazi hii. Mawaidha yangu kwenu nawaomba muwe mwanga na kielelezo bora kwa wasomi wengine kama mimi.

IKISIRI

Diwani ya *Howani Mwana Howani* ni Diwani ambayo imekusanya tenzi mbili ambazo ni *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Tenzi hizo zinazungumzia mila na desturi za Mwanamke wa Visiwani kuanzia alipobeba ujauzito mpaka alipoolewa na kupelekwa kwake. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alichunguza vipengele vya fani kama vile: matumizi ya lugha, mandhari na wahusika ili kuona ni jinsi gani mila na desturi za mwanamke wa visiwani zilivyojidhihirisha katika tenzi teule. Utafiti huu ulitumia mbinu ya maktabani. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Wateuliwa wa utafiti huu waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi lengwa. Aidha, data zilizokusanywa katika utafiti huu, zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaielezo. Utafiti huu umegunduwa kuwa tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* zimejedili kwa kiasi kikubwa mila na desturi za mwanamke wa visiwani. Mila na desturi hizo zimeanzia tokea mwanamke alipokuwa mja mzito, kipindi cha kujifunguwa, malezi ya mtoto wa kike, kipindi cha kubaleghe, kipindi cha ndoa, katika mavazi, mapambo, ngoma za asili, pamoja na tiba za asili. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Sosholojia katika kuelezea lengo mahsusi la kwanza na la pili na Nadharia ya Semiotiki imetumika katika kuchambua data zinazohusiana na lengo mahsusi la tatu, ili kufikia lengo la utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa vipengele kama vile mandhari, matumizi ya lugha pamoja na wahusika vimejitokeza kwa kiasi kikubwa katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*, vipengele hivyo vimesaidia sana katika kufikisha malengo ya Mwandishi ya kuelezea Mila na Desturi za mwanamke katika jamii ya visiwani Zanzibar.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKI MILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI	vi
IKISIRI	viii
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI WA JUMLA.....	1
1.1 Mada ya Utafiti	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	4
1.4 Malengo ya Utafiti	5
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti	5
1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti.....	5
1.4.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.5 Umuhimu wa Utafiti	6
1.6 Mipaka ya Utafiti	7
1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake	7
1.8 Mpangilio wa Utafiti.....	7
1.9 Hitimisho.....	8
SURAYA PILI.....	9
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA.....	9
1.1 Utangulizi.....	9

2.2	Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali	9
2.2.1	Dhana Kuhusu Mila	10
2.2.2	Dhana ya Desturi.....	13
2.2.3	Dhana ya Fani	16
2.2.3.1	Dhana ya Mandhari.....	17
2.2.3.2	Dhana ya Wahusika.....	18
2.2.3.3	Matumizi ya Lugha	18
2.2.3.3.1	Tamathali za Usemi	19
2.2.3.3.1.1	Tashibiha	19
2.2.3.3.1.2	Sitiari	20
2.2.3.3.1.3	Tashihisi	20
2.2.3.3.1.4	Tafsida.....	21
2.2.3.3.1.5	Misemo na Methali	21
2.3	Mkabala wa Kinadharia	22
2.3.1	Nadharia ya Sosholojia	22
2.3.2	Nadharia ya Semiotiki.....	23
2.4	Hitimisho.....	27
	SURA YA TATU	29
	MBINU ZA UTAFITI.....	29
3.1	Utangulizi.....	29
3.2	Umbo la Utafiti	29
3.3	Eneo la Utafiti	29
3.4	Ukusanyaji wa Data	30
3.4.1	Data za Msingi	30

3.4.2	Data za Upili	30
3.5	Mbinu za Kukusanya Data.....	31
3.5.1	Mbinu ya Usomaji Makini.....	31
3.5.2	Mbinu ya Upitiaji Nyaraka	32
3.6	Uteuzi wa Watafitiwa	32
3.7	Uteuzi Lengwa.....	32
3.8	Watafitiwa.....	33
3.9	Mkabala wa Uchambuzi wa Data	33
3.10	Hitimisho.....	33
SURA YA NNE.....		35
UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI.		35
4.1	Utangulizi.....	35
4.2	Muhtasari wa Kitabu Teule.....	35
4.2.1	Usuli wa Mwandishi	36
4.3	Kuainisha Mila na Desturi Katika Tenzi za Howani na Mwanakukuwa.....	38
4.3.1	Utangulizi.....	38
4.3.2	Malezi ya Watoto.....	38
4.3.4	Mafunzo/ Kufunda	39
4.3.5	Ndoa za Watu wa Visiwani.....	40
4.3.6	Elimu.....	40
4.3.7	Ngoma za Asili	40
4.3.8	Tiba za Asili.....	41
4.3.9	Mapambo/Urembo wa wanawake wa Visiwani	41

4.3.10	Mavazi ya Watu wa Visiwani.....	41
4.4	Uchambuzi Wa Data za Mila na Desturi Katika Tenzi Teule	42
4.4.1	Utangulizi.....	42
4.4.2	Uchambuzi wa Mila na Desturi Katika Utenzi wa Howani.....	43
4.4.2.1	Malezi ya Mimba na Kujifunguwa	43
4.4.2.2	Malezi ya Mtoto wa Kike	47
4.4.2.3	Masuala ya Elimu.....	52
4.4.2.4	Sherehe za Unyango	55
4.4.3	Uchambuzi wa Mila na Desturi Katika Utenzi wa Mwanakukuwa.....	56
4.4.3.1	Sherehe za Unyago.....	56
4.4.3.2	Ndoa za wanawake wa Visiwani	58
4.4.3.2.1	Kipindi cha Kutafuta Mchumba na Kupeleka Posa.....	59
4.4.3.2.2	Kipindi cha Kupeleka Mahari.....	63
4.4.3.2.3	Kipindi cha Kufunga Ndoa	67
4.4.3.2.4	Kipindi cha Baada ya Ndoa	72
4.4.3.3	Ngoma za Asili.....	78
4.4.3.4	Tiba za Asili.....	82
4.4.3.5	Mapambo/ Urembo wa Wanawake wa Visiwani.....	85
4.4.3.5	Mavazi ya Wanawake wa Visiwani	87
4.5	Mbinu za Kifani	89
4.5.1	Mandhari	90
4.5.2	Wahusika Katika Tenzi za Howani na Mwana Kukuwa	91
4.5.2.1	Kukuwa/ Sihadaike	92
4.5.2.2	Mama yake Kukuwa	94

4.5.2.3	Bibi Mkunga	96
4.5.2.4	Bi. Mrashi	97
4.5.2.5	Somo Yake Kukuwa	97
4.5.3	Matumizi ya Lugha.....	98
4.5.3.1	Tashibiha.....	99
4.5.3.2	Tashihisi	101
4.5.3.3	Tafsida.....	103
4.5.3.4	Sitiari	104
4.5.3.5	Misemo na Methali	104
4.6	Hitimisho.....	105
SURA YA TANO		106
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....		106
5.1	Utangulizi.....	106
5.2	Muhtasari	106
5.3	Hitimisho.....	111
5.4	Mapendekezo	112
MAREJELEO		114

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Mada ya Utafiti

Kutathmini mila na desturi za mwanamke wa visiwani katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*.

1.2 Usuli wa Mada

Neno Utamaduni si neno geni katika jamii ya wazawa wa Afrika Mashariki hususan Tanzania na Kenya. Neno hili hutumiwa katika sehemu mbalimbali za kawaida na katika maeneo ya kitaaluma. Neno utamaduni lina maana ya kilugha na kiistilahi. Neno hili kilugha pia lina asili ya Kiarabu lenye maana ya “mfumo wa maisha ya mtu au jamii fulani”. Kiistilahi kwa mujibu wa Taylor kama alivyonukuliwa na Omar (1981: 3) katika “*Urithi wa Utamaduni Wetu*” neno “utamaduni linajumuisha mambo mengi yakiwemo mila, desturi, lugha, itikadi, silka, imani, sanaa, maadili, na mazoea.”Hivyo neno utamaduni kwa kiasi kikubwa halipingani na fasili ya Teylor kwani ni “...maisha ya mtu au jamii katika mazingira maalum na ya asili yanayojumuisha lugha mama, imani, mila, maadili, itikadi, desturi, sanaa, michezo, na mazingira au watwani mahsusi. Kutokana na Omar (1981) “Utamaduni ni ile hali ya mienendo ambayo tunaendesha mambo yetu katika maisha ya jamii ya kila siku kama vile ufahamu wa elimu, imani, sanaa, maadili, sheria, mila na desturi n.k.

Kila jamii duniani inao utamaduni wake, na hivyo ndivyo ilivyo kwa jamii ya visiwani. Utamaduni ni jumla kuu inayokusanya mambo yote ya asili

yanayotendeka katika jamii hiyo. Mambo hayo ni kama vile : lugha, mila, itikadi, desturi, harusi, maziko, ngoma, dini, malezi, mavazi na hata tabia. Mazingira na historia huchangia sana mwelekeo wa utamaduni na kuusababisha uwe hivyo ulivyo. Mwinyi (2004).

Unguja na Pemba (Zanzibar) ni visiwa na kama ilivyo kawaida kwa visiwa vyote duniani, wenyeji wake hawakuchimbuka ardhini wala hawakuota kama mimea bali ni watu waliotokana na wahamiaji wa kale waliohama makwao kwa sababu mbalimbali na kuhamia Zanzibar Khamisi (2008). Baadhi ya wahamiaji hao walitoka nchi za jirani na wengine nchi za mbali kama vile nchi zote za pwani ya Afrika Mashariki na Afrika ya Kati, tokea Somali, Lamu, Mombasa, Mzizima, hadi Msumbiji. Wako waliotoka Madagascar, Ngazija, Yemen na hata Omani na Barahindi. Pia wako waliotoka Bara Kama vile Ujiji na Kongo. Jamii zote hizi ndizo zilizochangia katika utamaduni wa Mzanzibari na kuupa sura uliyonayo hivi sasa.

Mila na desturi ni vipengele mojawapo kati ya vipengele vinavyojenga utamaduni wowote ule duniani, vilevile ni nguzo muhimu sana katika utamaduni wa jamii yoyote ile. Mila huhalalisha matendo na taratibu katika jamii. Mtu akiwauliza watu kwa nini mnafanya jambo fulani, atajibiwa kuwa ni mila na desturi zetu kufanya hivyo, wakiwa na maana ya kuwa ni halali kwao kufanya hivyo. Kwa hiyo, mila ni sawa na sheria zilizoandikwa. Desturi hueleza namna jamii inavyoendesha mambo yake. Yaani namna ambayo kwa kawaida watu katika jamii hufanya mambo yao. Mila na desturi hujengwa, hukomaa, hurithishwa kutoka katika kizazi kimoja hadi kingine na pia huweza kufifia na kupotea.

Desturi huanza Kama tabia ya mtu au kundi la watu. Tabia hii ikimea kwa jamii nzima hugeuka na kuwa desturi. Desturi zikiota mizizi zikawa ndizo namna halali za kufanya mambo hugeuka kuwa mila. Kutokana na Khamisi,(2008), mila za Waswahili wa visiwani ni juu ya yale waliyoyaamini kuwa yanawaletea upendo wa kuishi kijamaa, kimitaa au kivijiji. Mfano kula kiukumbi, kuabudu pamoja n.k. na Desturi ni ada au mazoea ambayo watu wanayafanya kila siku kama vile mavazi, vyakula, uvuvi n.k. Miongoni mwa mila na desturi hizo zinapatikana katika tenzi za *Howani* na *Mwanakukuwa*.

Utenzi wa Howani na *utenzi wa Mwana Kukuwa* ni tenzi mbili zilizotungwa na mwandishi wa kike anaejulikana kwa jina la Zainab Himid Mohammed (2004). Tenzi hizi ni tenzi ambazo zinasimulia mila na desturi pamoja na mafunzo ya dini na dunia katika vipindi mbalimbali vya maisha ya mwanamke wa visiwani, kuanzia kuzaliwa kwake, utoto wake, avunjapo ungo na kuwa mwari, anapoposwa, kufungishwa ndoa na kuolewa, maisha ya ndoa na ulezi wa mimba. Hizi ni mila na desturi ambazo zinamuongoza mwanamke wa visiwani na kumfungamanisha na maadili ya jamii yake. Mila na desturi hizo katika tenzi husika zinajaribu kudokeza mafunzo ya nyumbani ambayo anayapata msichana katika vipengele vya jinsi ya kulea mimba na mtoto, kutunza mwili wake, kutunza siri za nyumba, kumtunza mume wake, kujuwa kazi za mikono pamoja na mapishi n.k.

Mila na desturi hizo zinzopatikana katika Tenzi teule, zimemsawiri muhusika wa kike katika nyanja mbalimbali. Kwa mujibu wa Ponera (2014), anasema kuwa usawiri wa wahusika ni kitendo cha kuwachora, kuwafafanuwa, kuwatambulisha na

kuwajenga wahusika huku wakipewa maneno, matendo, hadhi na uwezo unaolandana au unaowiana nao. Wakati tunapozungumzia wahusika, tunaona kuwa wako wa aina mbili nao ni wahusika wa kike na wa kiume. Katika utafiti huu tutachunguza mila na desturi katika usawiri wa wahusika wanawake wa visiwani kama ulivyoielezwa na mwandishi katika tenzi teule. Katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* mila na desturi ambazo mwandishi amezieleza zinampa uhuru muhusika wa kike. Mathalan katika tenzi hizo mwanamke anasawiriwa kama mtu mwenye kupenda umaridadi, mwenye kuendeleza na kudumisha mila, kama mzazi na mlezi, mwenye maarifa na ujasiri, mtibabu n.k.

Kutokana na maelezo hayo mtafiti ameamuwa kufanya utafiti huu kutokana na ukweli kwamba, hakuna tafiti nyingi zilizofanywa zinazoonyesha mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Mathalan mtafiti Mbayi (2009), alifanya utafiti unaohusu uhakiki wa fani katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* bila ya kuangalia vipengele vinavyohusu mila na desturi na kuonyesha jinsi vipengele hivyo vilivyoziyenga tenzi husika. Hivyo mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti ili kuona ni kwa namna gani mila na desturi za mwanamke wa visiwani zilivyosawiriwa katika tenzi teule.

1.3 Tatizo la Utafiti

Mila na desturi ni mtazamo wa kifikra unaotafautisha jamii moja na nyengine. Vilevile ni mfumo wa jamii unaofuata imani, maadili, desturi, tabia na sanaa ambazo jamii huzitumia kwa ajili ya kuongoza maisha yao ya kila siku, na kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kingine.

Watafiti mbalimbali kama vile Sengo (1985), Khamisi (2008), Ali (2015) wamewahi kufanya utafiti unaohusiana na mila na desturi za Waswahili wa visiواني. Hata hivyo, baada ya mtafiti kutalii kazi mbalimbali aligundua kuwa, hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kwa lengo la kutathmini mila na desturi za mwanamke wavisiواني katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Hivyo mtafiti ameona ipo nafasi ya kufanya utafiti huu ili kuziba pengo la kitaaluma katika uwaja wa fasihi ya Kiswahili.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utakamilika baada ya kukamilika lengo kuu moja na malengo mahsusi matatu ambayo ni haya yafuwatayo:

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Kuchunguza na kutathmini mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazojidhihirisha katika tenzi za *Howani* na *Mwanakukuwa*. Na mbinu za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi hizo.

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

- (i) Kuainisha mila na desturi zote zinazojitokeza katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*.
- (ii) Kuchambuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني, Zinazopatikana katika tenzi teule.
- (iii) Kubainisha mbinu zakifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika Usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi teule.

1.4.3 Maswali ya Utafiti

- (i) Je, ni mila na desturi zipi zinazojitokeza katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*?
- (ii) Ni mila na desturi gani katika usawiri wa mwanamke wa visiwani zinazopatikana katika tenzi teule?
- (iii) Je, ni mbinu zipi za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi teule?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ukishakamilika utakuwa na umuhimu ufuwatao : Kwanza, utakuwa ni marejeleo ya wanataaluma mbalimbali wanaofanya tafiti zao katika masuala ya fasihi ya Kiswahili hususan tenzi za Kiswahili.

Pili, wanafunzi wanaojifunza masuala ya Kiswahili watautumia utafiti huu katika kujifunza namna utenzi ulivyo na uwezo wa kusawiri mila na desturi katika jamii wanayoishi.

Tatu, watafiti wa masuala ya fasihi, utafiti huu utawasaidia kupata maeneo zaidi yakufanya utafiti katika kazi za mwandishi mteule.

Vilevile, wahadhiri wa vyuo vikuu na walimu mbalimbali watautumia utafiti huu kama marejeleo kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wao.

Mwisho, wataalamu wa masuwala ya utamaduni, pamoja na wanaharakati wanaohusiana na masuwala hayo, utafiti huu utawasaidia katika kutoa elimu kwa wasomaji kuhusu masuwala ya mila na desturi katika jamii zao.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi za *Howani na Mwana Kukuwa* zilizoandikwa na Zainab Himid Mohammed (2004). Mbinu iliyotumika kukusanyia data ni mbinu ya maktabani, pia data zilikusanywa, kuchambuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Katika kukamilisha lengo hilo, tumechunguza vipengele vya wahusika, lugha na mandhari jinsi vilivyoibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani. Nadharia zilizouongoza utafiti huu ni nadharia ya Sosholojia na Semiotiki.

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Hornsby (2000) anatoa maana ya vikwazo kuwa ni hali, tukio au kitu chochote ambacho kitakufanya upate ugumu katika kufanya au kulifikia jambo. Vikwazo vya utafiti ni jumla ya mambo yote ambayo yatamkwaza mtafiti katika kukamilisha utafiti wake.

Mtafiti wa utafiti huu alikumbana na vikwazo mbalimbali. Kikwazo kikubwa cha utafiti huu ni upatikanaji wa marejeleo yanayohusiana na mada inayotafitiwa.

Kwa kukitatuwa kikwazo hiki mtafiti alitumia mtandao wa intaneti ili kupata marejeleo yanayohusika. Aidha mtafiti alisafiri kwenda katika jiji la Dar-es-salaam ili kutafuta marejeleo ambayo yalimsaidia kuendeleza utafiti wake.

1.8 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu umegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti ambapo masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi

katika utafitihuu yamejadiliwa na kuzingatiwa. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wakinadharia. Mjadala katika sura hii unaibua pengo la kimaarifa, unajadili kiunzi cha nadharia na kufanya mjadala wa kina zaidi juu ya matumizi ya nadharia inayoongoza utafiti huu. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Katika sura hii tulionyesha mbinu za ukusanyaji data, mbinu za usampulishaji na kujadili mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne ni uchambuzi wa data ambapo data ziliwasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa katika mbinu ya uchambuzi wa kinaelezo. Sura ya tano, ambayo ndiyo sura ya mwisho, inahusu muhtasari wa matokeo, maoni na mahitimisho ya jumla ya utafiti huu.

1.9 Hitimisho

Sehemu hii imeeleza mambo ya msingi ya kiutangulizi, ambayo ni utanguluzi wa jumla wa utafiti wetu. Kama vile mada ya utafiti, usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo la utafiti, malengo mahsusi ya utafiti, maswali ya utafiti umuhimu wa utafiti, pamoja na vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti. Sura ya pili imeeleza mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.

SURAYA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

1.1 Utangulizi

Creswell (2009), anaeleza kuwa, utalii wa kazi tangulizi ni uchaguaji na ufupishaji wa utafiti kuhusu mada, anaendelea kueleza kuwa, hutoa muundo na kuonesha umuhimu kwa kulinganisha matokeo na utafiti mwengine. Utafiti sio kazi ya kulala na kuamka humlazimu mtafiti kuhangaika huku na kule ili aweze kufanikisha kazi yake. Ndani ya utalii wa kazi tangulizi, hupatikana nadharia za utafiti, nadharia ya njia ya utafiti, nadharia ya uchambuzi wa data. Aidha utalii huo wa kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa kuzamia mbizi maandishi hayo ya huko nyuma na kufananishwa na taarifa hai zipatikanazo katika utafiti wa sasa na data za awali zitokanazo na usaili wa ana kwa ana, ama data za majibu ya mahojiano, (Sengo 1985).

Baada ya kuelezea kazi ambazo zimeandikwa zinazohusiana na mada ya utafiti huu, mtafiti ameelezea nadharia ya Sosholojia na Semiotiki ambazo zilimuongoza katika utafiti huu.

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

Katika sehemu hii mtafiti amefanya ufafanuzi wa istilahi mbalimbali zinazojitokeza katika utafiti huu. Istilahi hizo ni: mila, desturi, fani, wahusika, mandhari na lugha vipengele vya lugha vilivyojadiliwa ni misemo na methali, tamathali za usemi, na tamathali za usemi ambazo zitatumika ni tashibiha, sitiari, tafsida na tashihisi.

2.2.1 Dhana kuhusu Mila

Mila za wanawake wa visiwani ni juu ya yale waliyoyaamini kuwa yanawaleta upendo wa kuishi kijamaa, kimtaa, au kivijiji. Mfano kula kiukumbi, kuabudu pamoja na kusaidiana kiuvyawa au kiujima kwa malezi, uuguzi, ndoa, tiba, wakati wa msiba na furaha. (Khamis 2008). Mila hizi kwa wanawake wa visiwani zinawapa faraja ya kuishi vyema ingawa hali zao ni maskini. Baadhi ya wanawake wa visiwani wana mila ya kufanyiana uchawi kwa lengo la kuhusudiana kwa kurogana, kupeana pungu, mashetani, majini, kupelekeana chui, vizuu na kuwangiana. Watu hao hutofautiana namna ya kufanyiana uhusda huo.

Kamati ya tamasha ya utamaduni wa jamii ya Wairaqw na Wagorowa Wilaya ya Babati waliandika makala kuhusiana na *Historia ya Chimbuko, Mila na Desturi za kabila la Wagorowa*. Katika makala yao wanasema kuwa wanawake wa Kigorowa walivaa mavazi ya ngozi mbili zilizolainishwa na kutengenezwa vizuri na zenye vitundu vidogovidogo. Viatu vyao ni vya ngozi za wanyama vilivyotengenezwa vizuri kwa kamba ya kushikilia miguu. Mapambo ya asili ya mwilini ni kama vikuku vya shaba nyeupe au njano, vikuku vya pembe za tembo, hereni na shanga za ukubwa mbalimbali. Wagorowa walitumia rangi ya bluu iliyopatikana katika majani fulani kwa ajili ya pambo la midomo. Vilevile walitumia mizizi kama tiba ya magonjwa mbalimbali. Mizizi hiyo ilichemshwa na kupondwapondwa na wagonjwa kunyweshwa maji baada ya kuchujwa. Watoto wa kike na wa kiume wa Kigorowa wanapozaliwa na kukuwa hufundishwa maadili mema ya kuishi na jamii. Mtoto wa kike hufundishwa na akina mama maadili mema ya kuishi na mume na namna ya kutunza familia anapoolewa

na kuzaa. Wagorowa hufanya tohara kwa watoto wa kike na kiume, na sherehe kubwa hufanyika wakati vijana wanapoingia katika jando na unyago. Ndoa zao hufanyika kwa makubaliano kati ya waozaji wa mtoto wa kike na wa kiume. Kwa kawaida mahari yanayolipwa ni dume wadogo watatu, kubwa moja, pia vinywaji hunywewa wakati wa sherehe. Ingawa makala haya hayahusiani moja kwa moja na kazi inayofanyiwa utafiti, yalitusaidia sana katika kupeleka mbele uchambuzi wa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi teule.

Hussein (2014), katika tasnifu yake ya umahiri, aliandika kuhusu “Uchunguzi kuhusu mchango wa nyimbo na masimulizi ya matambiko katika kurithisha mafunzo, mila na desturi za Wakaguru wa Mamboya”. Katika hitimisho lake amesema kuwa, Wakaguru walizitumia sana nyimbo hizo kutolea maadili hasa kwa vijana na kuwarithisha mila na utamaduni wa jamii yao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ingawa utafiti wake hauhusiani na mada inayotafitiwa, lakini umetusaidia sana kupeleka mbele mada tunayoifanyia utafiti.

Swaleh (1992), katika Tasnifu yake ya umahiri ameshughulikia maudhui katika Utenzi wa *Mwanakupona*. Katika uhakiki wake, amesema kuwa maudhui ya dini yamejikita katika mafundisho ya dini ya Kiislamu yanayomtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Swaleh anaendelea kusema kuwa hadhi anayopewa mwanamke katika jamii yake inastahiki. Mtafiti huyu anadai kuwa majukumu apewayo mwanamke kwa jamii, ndiyo yanayochangia kumdhulumu. Kazi ya mtafiti huyu ilitufaa katika kuchumguza mila na desturi katika usawiri

wa mwanamke wa visiwani katika tenzi teule, ingawa haihusiani na kazi inayofanyiwa utafiti.

Dezidery (2010), aliandika makala inayohusiana na *Utenzi wa Mwanakupona*. Katika makala yake alichambuwa nafasi ya mwanamke katika kumtunza mumewe. Dezidery anaeleza namna mwanamke anavyotakiwa kumfanyia mumewe mambo mbalimbali, miongoni mwa mambo hayo ni: kutojibizana naye, kumpa kila anachokihitaji, kumuaga vizuri kila anapoondoka, kumpokea vizuri kila anaporudi, kumpapasa na kumpepea usiku, kumkanda mwili na kumsifu kwa watu wengine, kumnyowa ndevu na kumpendezesha. Makala hii imetusaidia sana katika kuchunguza mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani, ijapokuwa haihusiani moja kwa moja na kazi tunayoifanyia utafiti.

Khatib (1985) katika *Mulika*, aliandika makala inayohakiki *Utenzi wa Mwanakupona*. Katika maelezo yake anaeleza kuwa utenzi wa *Mwanakupona* ni sumu mbaya inayorejesha nyuma maendeleo ya “MWANADAMU” kwa kumuingiza mwanamke utumwani. Kwani kumtenga mwanamke na shughuli za kiuchumi katika mfumo wa kimaisha wa kibinafsi, kumtumikisha katika tume za sulubu na upishi ni kumfunga pingu za utawa na uduni wa ndoa, ni pigo kubwa kwa umma mkubwa wa kike duniani. Katika hitimisho lake anasema kuwa, *Utenzi wa Mwanakupona* ni utenzi unaobaki kama kielelezo kizuri kitaaluma kilichoghoshi utamaduni wa upwa, Uislamu na bidaa zake. Kwa msaada wa utungo huu nafasi ya mwanamke katika unyonge wake, uonevu wake, na shida zake, imeoneshwa bila kificho. Lakini juu ya uzuri huo,

jamiiya leo na hasa jamii ya kimaendeleo inayojengwa Tanzania, mwanamke anatakiwa apewe hadhi inayostahiki. Asiwe mtawa, mfariji kimwili kwa mume au mtumishi nyumbani. Mwanamke aoneshwe kuwa mtu aliye sawa na mwanamke katika jamii na ashirikishwe kikamilifu katika harakati za maisha hasa katika harakati za uzalishaji mali. Tunamuunga mkono Khatib katika mawazo yake ya kutaka kumkombowa mwanamke na kumtoa katika utumwa aliopewa katika ndowa. Ingawa makala haya hayahusiani na kazi inayofanyiwa utafiti, kazi hii imetusaidia sana katika kuchambuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi zilizoteuliwa.

2.2.2 Dhana ya Desturi

Desturi ni ada na mazoea ambayo watu wanayafanya kila siku. Khamis (ameshatajwa). Wanawake wa visiwani wana desturi nyingi zikiwemo zifuwatazo: Kimavazi wanawake wa visiwani mavazi yao ni kanzu, shumizi, buibui, kanga, kaniki, gwaguro, mitandio, sidiria na viatu vya ngozi. Ziada ya mavazi yao wana desturi ya kujipamba kwa vyombo vya dhahabu, fedha na kareti, kama bangili, vidani, vipini, pete, herini, n.k. Aidha hutengeneza vikuba na mapambo mengine kwa kutumia mauwa yanayonukia kama vile: mkadi, asumini, vilua na mawaridi. Wanawake hawa hujitona kwa hina na podari, hujipamba kwa behedani, rangi za mdomo, mafuta mazuri na haliudi, miski pamoja na kijifukiza udi wa mawaridi, pale wanapotoka nyumbani, wanapokwenda harusini, safari ya matembezi au hata kazini. Baadhi ya wanawake huwasinga waume zao kwa kutumia liwa na karafuu au dawa za kienyeji zinazonyoosha au kutakatisha mwili.

Kwa upande wa vyakula wanawake wa visiwani wana desturi ya kupika vyakula vya nazi kama vile: muhogo, viazi vikuu, wali, ndizi majimbi n.k. Baadhi ya vyakula hivyo havitimii kuliwa kwake mpaka vipate mboga na mchuzi au kitoweo. Vitoweo hivyo huwa ni vya samaki au nyama.

Wanawake wa visiwani wana desturi ya kufanyiana utani hususan katika harusi, siku moja au mbili kabla ya harusi. Au ile siku ya harusi hasa. Wanawake hawa huwa na utani wa kuufunga mlango wa chumba cha Bibi. Harusi, humfunika kanga Bibi. Harusi na wapambe wake wengine, na kutakiwa Bwana Harusi amuaguwe mkewe na anapokosea hutakiwa atowe fidia kwa kutoa kiasi cha pesa. Katika kipengele cha tiba wanawake wa visiwani hutumia dawa za mitishamba kwa baadhi ya magonjwa baada ya kupelekana hospitali.

Ali (2015) alichunguza nafasi ya mwanamke wa Kipemba kama inavyosawiriwa katika hadithi simulizi za uswahilini Pemba. Katika hitimisho aligundua kuwa mwanamke wa kisiwa cha Pemba ni mlezi, mchapakazi, mvumilivu, moga, mwenye kuonewa na asiye na ukweli. Ingawa utafiti huu ulihusu kazi tofauti na kazi iliyotafitiwa, hata hivyo utafiti huu ulimuongoza mtafiti namna ya kuchunguza mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani zilivyojidhihirisha katika kazi teule.

Kivenule (2013), aliandika makala inayohusiana na mila na tamaduni za kabila la Wahehe, katika mkoa wa Iringa. Katika maelezo yake anasema kuwa kabila la Wahehe katika masuala ya uchumba huangalia mambo mbalimbali ikiwemo tabia ya uchapaji kazi hususan kilimo na kuangalia kama ana uwezo wa

kuimarisha familia. Posa ikikubalika, upande wa mwanamme hutoa jembe kama kitanguliza uchumba (mkaja). Mwanamke anapopata mimba akiwa ndani ya ndoa baada ya miezi saba tangu aolewe, mama yake anaenda kuomba ruhusa kule alikoolewa ili akaishi nae hadi siku atakapojifunguwa, na baada ya kujifunguwa hurudishwa kwa muumewe. Ingawa makala hii haihusiani na utafiti wetu, imetusaida sana katika kuchambua mila na desturi katika usawiri wa mwanawake wa visiواني Zanzibar katika tenzi teule.

Naye Ngonyani (2010), aliandika makala inayohusiana na mila na desturi za Wangoni katika upande wa ndoa na kuchumbia. Katika makala hiyo amesema kuwa katika kabila la Wangoni hapo zamani kijana na msichana walipofikia umri wa kuo na kuolewa walifanya hivyo. Anaendelea kusema kuwa katika kabila hili ndoa haifungwi katika ukoo mmoja (ndugu) kwa sababu ya kuogopa watoto watakozaliwa kuwa watakufa au watapata kifafa au pengine mababu (mahoka) watakasirika. Mtoto wa kiume anapotaka kuowa wazazi wengine walimtafutia mke na wengine walimuacha atafute mwenyewe amtake. Makala hii ili msaidia mtafiti kuchunguza mila na desturi za mwanamke wa visiواني katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukua*, japokua makala hii haikuhusiana moja kwa moja na utafiti huu.

Mulokozi (1999), alifanya uhakiki katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Katika uhakiki wake anaeleza kuwa, *Utenzi wa Mwanakupona* ni Utenzi unaowakilisha vizuri tungo za utamaduni na mawaidha zinazowahusu Waafrika. Anasema kuwa Waafrika wanazo mila na desturi zao za jadi kuhusu mahusiano ya watukatika

ndowa na maisha kwa ujumla, ambazo huwafundisha watoto wao. Mafunzo hayo, kwa watoto wa kike, kijadi yalikuwa yakitolewa katika unyago, ngano na masimulizi mengine, na katika matendo ya kimila ya kila siku.

Adabu na heshima, kujiheshimu, kuepuka umbeya na fitna, kutokuwa mchoyo, kuwa msafi, kuishi na watu vizuri, n.k, ni baadhi ya mambo ambayo mabinti wa Kiafrika hufundwa, na baadhi yao tunayakuta katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Ingawa uhakiki huu ulihusu kazi tofauti na kazi iliyotafitiwa, hata hivyo utatuongoza namna ya kuchunguza mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi teule.

2.2.3 Dhana ya Fani

Wataalamu na wahakiki wa fasihi kama vile Wamitila (2002), Njogu na Chimera (1999), wanakubaliana kuwa, fani ni jumla ya viamba jengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Mathalan Wamitila (ameshatajwa), anasema kuwa, fani hutumika kueleza muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha maudhui yaliyomo. Senkoro (1982) anasema kuwa fani katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake.

Katika utafiti huu, mtafiti ameshughulikia baadhi ya vipengele vya fani vinavyojidhihirisha katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*, vipengele hivyo ni mandhari, wahusika na lugha.

Faki (2015) alifanya uchunguzi wa sifa za kifani za utendi wa Kiswahili mfano: *Utendi wa Fumo Liongo*. Ili kufikia hitimishi lake alifanya uchambuzi juu ya vipengele vya muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Ingawa utafiti huu haukuwa na nia ya kuchunguza mila na desturi za mwanamke wa visiwani, hata hivyo umetusaidia katika kusukuma mbele kazi hii kwa sababu umeonesha namna ya kufanya uchambuzi wa data zinazohusiana na lugha, wahusika na mandhari.

Mbayi (2009), alifanya utafiti kuhusiana na Uhakiki wa fani katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Vipengele vya kifani alivyovishughulikia ni wahusika, mandhari, toni, wakasi, usimulizi, msuko, umbo na lugha na kuvionesha jinsi vinavyotumika katika uhakiki wa kifani. Japokuwa utafiti huu hauhusiani na mada inayotafitiwa utatusaidia katika kukamilisha lengo mahsusi la tatu.

2.2.3.1 Dhana ya Mandhari

Mandhari ni mazingira ya utendaji au usimulizi. Matendo yanayofanyika katika kazi ya fasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalum. Hivyo basi mandhari ni ile elementi katika kazi ya fasihi inayomuwezesha msomaji kujuwa wapi au lini matukio yanayowasilishwa yalitendeka. Gills (1985) akinukuliwa na Pauline (2013) anasema mandhari ni dhana pana na jumuishi. Anaungwa mkono na Wamitila (2008), anayejumuisha dhana ya mazingira, mawanda na wakati ndani ya mandhari. Kwao, mandhari si mazingira ya kijiogarafia tu bali hurejelea masuala mengine kama vile kipindi cha matukio au mwanda wa matukio kama inavyodhihirishwa na matendo ya wahusika. Maelezo ya wataalamu hawa ni

muhimu katika kuelezea suala la mandhari katika utanzu wa ushairi. Mandhari huweza kuhusishwa na mashairi ikiwa ushairi huo ni wa kisimulizi (Kama tenzi au tendi) Wamitila (2008).

2.2.3.2 Dhana ya Wahusika

Wahusika hufafanuliwa kama watu, wanyama, au vitu katika fasihi (Msokile 1992:43). Wahusika husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Wahusika wa kazi ya sanaa huwa na tabia zinazohusiana kati yao kwa sababu mbalimbali. Kwanza kabisa hutegemea mwandishi ana lengo gani analotaka kuonesha katika kazi yake ya sanaa. Pili, aina ya kazi ya sanaa inaweza kuathiri aina ya wahusika jinsi walivyosawiriwa, kuaminika kwao, wanavyohusiana wao kwa wao, uwakilishi wao na majina yao. Wamitila (2008:45) anasema wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu wahusika ndio jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika.

Kulingana na Njogu na Chimera (1999:45) wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Hivyo basi wahusika wa aina yoyote wawe watu au viumbe hurejelea na huwakisi sifa na tabia za banaadamu.

2.2.3.3 Matumizi ya Lugha

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) anaeleza kuwa matumizi ya lugha katika utenzi ni ya kipekee kulinganisha na matumizi ya lugha katika tanzu nyenginezo.

Lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa katika kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Moja kati ya kipengele cha lugha ni tamathali za usemi. Hivyo katika utafiti huu tumechunguza vipengele vya lugha ambavyo vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyengine ili kuwasilisha ujumbe uliyokusudiwa kwa hadhira.

2.2.3.3.1 Tamathali za Usemi

Tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana kwa dhana nyengine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza, au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtunzi. Mulokozi na Kahigi (1979), Tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, matonimia na sitiari.

Kahigi (1994) anadai kuwa msingi wa tamathali za useminyingi ni uhamishaji wa maana. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibuwa maana ya kiashiria (neno, fungu n.k) kutokana na maana ya kiashiria kingine. Katika utafiti huu mtafiti amechambua tamathali za usemi zifuwatazo: tashibiha, tashihisi, tafsida na sitiari. Mtafiti amezichaguwa hizo kwa sababu ndizo zinazojitokeza sana katika tenzi alizozichaguwa.

2.2.3.3.1.1 Tashibiha

Kahigi (1994), anafasili tashibiha kuwa ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno kama, mithili ya, kama kwamba, n.k. Naye Senkoro (1982), anaifasili tashibiha kuwa ni tamathali ambayo watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu

ama vitu vyengine kwa kutumia maneno kama mithili ya, kama kwamba, mfano wa na mengine ya aina hiyo. Mfano, Bwana Mussa ni mweusi kama mkaa. Hivyo ukitazama fasili hizo utaona kuwa wataalamu hao wanakubaliana kwa pamoja kuwa tashibiha hulinganisha vitu ama watu kwa kutumia maneno kama vile mithili ya, kama, mfano wa n.k.

2.2.3.3.1.2 Sitiari

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), sitiari ni tamathali ya ulinganishi bila ya kutumia viunganishi vya kulinganisha kama vile; “kama,” “ja,” `mfano wa`, na `mithili ya` TUKI (1984), wanasema kuwa, sitiari ni tamathali ya usemi inayohusisha vitu au viumbe viwili vilivyotafauti kitabia au kimaumbile kwa msingi wa sifa, iliyo katika vyote viwili, lakini, ulinganishi huo, haujitokezi waziwazi, kwa sababu ya kutotumia vilinganishi kama vile, mfano, mithili ya, n.k. Matumizi ya sitiari hujenga picha fulani katika ubongo wa msikilizaji au msomaji.

2.2.3.3.1.3 Tashihisi

Senkoro (1982) anafasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine. Huitwa fasili ya binadamu. Kwa sababu tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Mfano nyota zilikuwa zikitabasamu huku zimemzunguka mama yao. Sambamba na Senkoro, Kahigi (1994) anafasili tashihisi kuwa ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishwa kwenye kitu kisicho na uhai au dhahania (pengine tashihisi huitwa uhaishaji) Katika mfano huo nyota zimepewa sifa ya kibinadamu ya kutabasamu na kuzunguka.

2.2.3.3.1.4 Tafsida

Tafsida ni tamathali ya usemi ambapo neno, kirai, kishazi au sentensi ambayo maana yake haipendezi kutajwa hadharani, huondolewa na kuwekwa neno, kirai, kishazi, au sentensi nyengine inayotumika kurejelea dhana ileile. Low (2011). Tafsida inakusudia kuficha maana halisi, kuburudisha na hata kupotosha wakati mwengine. Neno, kirai, kishazi, au sentensi inapotumika kama tafsida maana yake ya kawaida hupotea na huwa na maana ya kitamathali. Mara nyingi matumizi ya tafsida huonesha ustaarabu wa mtu.

2.2.3.3.1.5 Misemo na Methali

Vipengele vyengine muhimu katika kigezo cha fani katika lugha ni misemo na methali. Vipengele hivi zaidi ya kuipamba lugha ya kazi ya fasihi kwa kuipa kazi hiyo “usanii” pia vinazo sifa nyenginezo muhimu zinazoongeza ukamilishaji wa kazi mbalimbali za fasihi. Omari na wenzake (1997) wakinukuliwa na Senkoro (1982) wanasema kuwa methali ni sehemu ya lugha ambayo inaweza kufananishwa na kiungo cha lugha na kitoweo cha lugha pia... Hutumiwa kwa kuyatafakari na kuyapima maisha, kufunzia jumuiya na kutawalia jamii na mazingira ya binaadamu.

Kulingana na Senkoro (ameshatajwa), misemo ni maneno yanayotumika mara kwa mara kuelezea maisha kama yalivyo katika mazingira maalum na kuleta maana maalum. Matumizi ya misemo katika kazi ya fasihi hufanana sana na yale ya methali. Misemo wakati mwengine hutumiwa kutambulisha mazingira maalum au kujulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa.

Jambo hili hutokana na sababu kuwa misemo huzuka na kutoweka kufuwatana na hali mbalimbali za kimazingira.

2.3 Mkabala wa Kinadharia

Kwa mujibu wa Sengo (2009), nadharia ni wazo kuu, muongozo mkuu wa mtu au wa jamii, wa pahala na wa wakati. Mtafiti wa kazi hii ameongozwa na nadharia ya sosholojia na nadharia ya semiotiki ili kukamilisha malengo ya utafiti wake.

2.3.1 Nadharia ya Sosholojia

Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Mmarekani anaeitwa Adam Smith mnamo mwaka (1970). Mwananadharia huyu anaeleza kwamba, nadharia hii imejikita zaidi katika kuangalia uhusiano wamwanadamu na mazingira yake. Maherey,(1978), Eaggleton (1983), kama walivyonukuliwa na Wamitila (2003), wanaeleza kuwa, wahakiki wa kisosholojia wanaamini kuwa kazi ya kifasihi inadhibitiwa na muundo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia wahakiki hawa wanaamini kuwa, jinsi wasomaji wanavyoipokea, kutathmini na kuihukumu kazi fulani huathiriwa pia na mazingira ya wasomaji hao kiwakati na kimahali. Msokile (1992), anaendelea kufafanua kuwa nadharia ya sosholojia hukubali kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii. Nadharia hii inaamini kuwa uhusiano wa kazi ya kifasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikiwa ni muhimu sana. Anaendelea kufafanua kuwa sanaa haijengwi katika ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati maalum akiwajibika kwa jamii inayomuhusu ambayo ni sehemu yake muhimu. Msokile (1993 : 4), anazidi kufafanua kuwa mkabala huu kimsingi hutawaliwa na imani kuwa uhusiano kati

ya kazi ya kifasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Mhakiki wa kisosholojia kihistoria huiweka kazi yake katika ulimwengu wa kijamii na halafu huelezea uhusiano uliopo kati yake. Kama uhusiano ni mdogo basi tathmini juu ya ubora ama udhaifu hufuata. Mazingira ya jamii ndio huweza kubadili maudhui ya kazi ya fasihi.

Nadharia hii imetumika katika utafiti huu kwa sababu mila na desturi za mwanamke wa visiwani ni miongoni mwa mambo yaliyomo katika jamii. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza na kuchambua mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani zinazopatikana katika tenzi za *Howani na Mwanakukuwa*. Udhaifu wa nadharia hiini kuwa huchunguza kipengele cha maudhui tu katika kazi ya fasihi, wala haijijhusishi na vipengele vya fani. Kutokana na sababu hiyo mtafiti alitumia nadharia ya semiotiki kwa lengo la kuziba pengo hilo.

Nadharia hii imetumiwa na Hamad (2014), ambae ameeleza kuwa kazi ya mwanasosholojia ni kuielewa jamii ambapo huangalia uhusiano wa jamii katika mienendo yao ya kila siku. Kwa hivyo, utafiti huu unategemea kuangalia mila na desturi katika usawiri wa wanawake wa jamii ya visiwani (Zanzibar). Kwa kutumia nadharia ya sosholojia.

2.3.2 Nadharia ya Semiotiki

Wataalamu mbalimbali wa kiisimu na kifasihi wametowa fasili tofauti tofauti za semiotiki. Baadhi ya fasili hizo ni:

Massamba (2004:76), anaeleza kuwa semiotiki ni taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na uchunguzi na uchanganuzi wa mfumo wa ishara mbalimbali ikiwa inazingatia zaidi uhusiano baina ya kiwakilishi na kiwakilishwa. Semiotiki ni taaluma ya mipangilio ya ishara inayomuwezeshabinadamu kuona vitu au hali kama ishara zenye maana. Njogu na Wafula (2007). Mifumo hii ni sehemu ya utamaduni japo imekabidhiwa mipaka maalum na maumbile kama lugha.

Waasisi wa semiotiki ni Saussure ambae amehusishwa na umuundo na Charles Pierce, mwanafalsafa Saussure anaegemea zaidi dhima ya ishara katika jamii, naye Pierce anazungumzia jinsi ishara zinavyohusiana kimantiki ili zilete maana maalum. Kulingana na mawazo ya Pierce ishara hutumiwa kufafanulia vitendo maalum na maana ya ishara hiyo inatokana na sheria fulani za utamaduni wa tanzu za lugha. Unakidi wa ishara hufanyika katika utamaduni mahsusi ambapo mifumo ya ishara inajulikana, inatumiwa na kufahamika na wanajamii waliotelewa katika utamaduni huo maalum. Mazoea ya lughayaliyodhihirishwa kuwepo kwa hakika ni msimbo wa utamaduni unaohusika, Scholes (1974).

Nadharia ya semiotiki ina uhusiano mkubwa na nadharia ya umuundo. Semiotiki inazungumzia uashiriaji wa vipashio vya lugha au tamathali nayo nadharia ya umuundo inahusu jinsi ishara zinavyowekwa kwa utaratibu unaoziwezesha kufahamika. Wamitila (2003), alieleza kuwa semiotiki ni aina ya nadharia ya kimuundo inayojishughulisha na ishara na maana za ishara hizo katika kazi ya kifasihi. Semiotiki huangazia uashiriaji na jinsi kazi za kifasihi zinavyowasiliana na wasomaji. Nadharia hii aidha huchunguza kwa nini kazi za

kifasihi zina maana zilizonazo kwa wasomaji wa kazi hizo. Maelezo hayo ya Wamitila kuhusiana na semiotiki ambayo yanaegemea katika uwanja wa fasihi yanatupa mwangaza mkubwa katika kuchanganua matumizi ya ishara katika diwani ya *Howani* na *Mwana Howani*.

Kuzuka kwa nadharia ya semiotiki kunahusishwa na miaka ya 1970 wakati ambapo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuwacha umuundo uliokuwa umeutawala uhakiki wa kazi za fasihi katika miaka ya 1960. kulingana na Wamitila (2002:178-179) Desaussure alifafanua lugha kama mfumo wa ishara ambazo huangaza na kuunda “mkufu wa ishara”.

Nadharia ya Semiotiki haiwezi kukamilika bila ya kurejelea mawazo ya Barthes (1968) kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambayo imeacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiraji katika kazi za kifasihi. Misimbo hii ni miongoni mwa nguzo kuu za nadharia ya semiotiki. Barthes alidhamiria kugawanya kazi ya kifasihi katika vitengo vidogovidogo vyenye urefu sawa alivyoviita leksia na kwamba kila leksia ilidhihirisha kaida yake muhimu katika kuifasiri. Barthes alifafanua misimbo ifuwatayo:

- a) Msimbo wa matukio: Unahusu namnamatukio yanayopatikana katika hadithi yanavyofuwatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi.
- b) Msimbo wa kihemenetiki: Msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi kwa hivyo huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anuwani ya kazi.

- c) Msimbo wa ki-seme: Hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi.
- d) Msimbo wa kiishara: Unahusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihi.
- e) Msimbo wa kiurejelezi: Hujengwa kutokana na viashirii vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi ya fasihi. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni. Msemaji akisema kuwa anakielewa kitu anachokimaanisha msanii husema hivyo katika msingi wa kiurejelezi au kiutamaduni. Msimbo huu wa kiurejelezi utatufaa sana katika kuchanganua viashirii vya kiutamaduni katika Diwani ya *Howani Mwana Howani*.

Waasisi wa Nadharia ya semiotiki wa Ki- Swiz Saussure na mwanafalsafa wa Kipragmatiki kutoka Marekani kwa jina la Pierce (Wamitila, 2002:132), na baadae wataalamu wa kiuumbaji, Voloshnov, Bakhtin na Derida ni wahakiki wa hapo baadae walioisukuma mbele nadharia ya semiotiki.

Katika kuchanganua matumizi ya kipengele cha fani katika Diwani yetu ya *Howani Mwana Howani*, tumetumia nadharia ya semiotiki kwa sababu tanaamini kuwa inafaa zaidi katika kujibu lengo letu mahsusi la tatu. Katika utafiti wetu huu tumerejelea baadhi ya mawazo ya wanasemiotiki kwa mujibu wa wataalamu na waandishi mbalimbali. Udhaifu wa nadharia hii ni kuwa huchunguza kipengele cha fani tu katika kazi ya fasihi, wala haijijhusishi na vipengele vya maudhui. Kutokana na sababu hio mtafiti alitumia nadharia ya sosholojia kwa lengo la kuziba pengo hilo.

Otoro (2012), alichambua “*msimbo na maana katika Zilizala*” akitumia nadharia ya semiotiki. Alifafanua kwa undani aina tano za misimbo hiyo kama zinavyojitokeza katika *Zilizala*. Alitumia mawazo ya Barthes (1974) kuhusu msimbo wa kisimulizi, kihemenetiki, msimbo wa kiutamaduni, msimbo wa kiishara na msimbo wa kihusika. Katika kushughulikia mada yetu msimbo wa kiutamaduni utakuwa wenye manufaa katika utafiti wetu kwa kuchanganua matumizi ya ishara katika *Howani* na *Mwana Kukuwa*.

Simon (2014), katika uchanganuzi wa kifasihi wa baadhi ya fani katika “*Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo*” alijishughulisha na nadharia ya semiotiki kwa kuchanganua ishara teule za kimtindokama anuwani, mandhari, wahusika na tamathali za usemi kama vile polisemia, taashira, sitiari, kinaya cha kitashtiti, chuku, taaswira na daiolojia kwa kutumia ishara na kiashirii pamoja na misimbo ya kiishara na kihemenetiki bila ya kutumia msimbo wa kiutamaduni kwa kuegemea mwanaisimu Saussure kuhusu kiashirii na kiashiriwa.

Pia ameangalia mawazo ya mwanafalsafa wa Kimarekani Pierce kuhusu kielelezo cha ishara chenye pembe tatu yaani ishara, yambwa na kifasiri. Katika utafiti wetu huu tumetumia msimbo wa kutamaduni (kiurejelezi) katika kukamilisha lengo letu mahsusi la tatu.

2.4 Hitimisho

Sehemu hii imeeleza fasili za dhana mbalimbali ambazo zimetumika katika utafiti husika. Fasili hizo zimepatikana kwa kutumia machapisho, vitabu, makala,

majarida na tasnifu ambazo mtafiti alizipitia na kupata uelewa wa kina kuhusiana na dhana husika. Vilevile sehemu hii imeeleza nadharia ya sosholojia na semiotiki ambazo zilimuongoza mtafiti katika kukamilisha utafiti wake. Sura ya tatu inahusiana na mbinu za utafiti. Eneo la utafiti, ukusanyaji wa data, pamoja na sampuli na usampulishaji.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti kukusanya na kuchambuwa data zitakazomuwezesha kufikia lengo la utafiti husika, Enon (2008).

3.2 Umbo la Utafiti

Utafiti huu umetumia umbo la kimaielezo Enon (2008) anaeleza kuwa umbo la kimaielezo ni njia ya kukusanya data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaielezo. Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaielezo. Mtafiti amechaguwa mbinu hii kwa sababu ameona itamuwezesha kufikia lengo la utafiti huu. Mbinu hii imetumiwa na mtafiti kuzichambuwa data kwa njia ya maelezo kwa kutegemea malengo mahsusi.

3.3 Eneo la Utafiti

Babbie (1992) anaeleza kuwa, eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyika au unakusudiwa kufanyika. Katika eneo la utafiti ndipo ambapo data zinazohusu utafiti husika zinapatikana. Hii ni kutokana na mtafiti kutumia njia moja kati ya njia nyingi za kukusanyia data, kama vile: mahojiano, kushuhudia, usaili, kushiriki shughuli au tukio hilo pamoja na mtafitiwa.

Hivyo utafiti huu ni utafiti wa maktabani ambao ulifanyika katika maktaba ya Wilaya ya Wete, maktaba kuu ya Pemba iliyopo Chakechake, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Tawi la Pemba, maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyoko Dar es salaam, maktaba ya Chuo Kikuu cha

Dar es salaam, pamoja na maktaba ya TATAKI. Maeneo hayo yalitumiwa na mtafiti kwa sababu utafiti huu ni wa maktabani. Pia, mtafiti ameona sehemu hizo zimemuwezesha kupata data za utafiti wake

3.4 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti wowote ule wa kitaalamu huwa kuna data za aina mbili, data za msingi na data za upili. Data zilikazokusanywa katika utafiti huu ni data za msingi na za upili. Utafiti huu ulizitumia data hizo ili kufikia madhumuni ya utafiti wetu.

3.4.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine kwa lengo la matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza Furlong (2000). Data za msingi za utafiti huu ni mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani na zilikusanywa kutoka katika kitabu cha *Howani Mwana Howani* (2004) kilichoandikwa na Zaynab Himid Mohammed.

3.4.2 Data za Upili

Kutokana na Kothari (2004) anasema kuwa data za upili ni aina ya data ambazo tayari zimeshakusanywa na watu wengine, ambazo tayari zimeshapitia katika mchakato wa kitarakimu na kimaelezo. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yaliyopatikana katika maktaba mbalimbali zilizoteuliwa. Katika maktaba hizo, mtafiti alisoma makala, ripoti,

tasnifu, majarida, vitabu vya maandishi pepe katika tovuti na wavuti zilizohusiana na mada inayotafitiwa.

3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Katika kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu za msingi na mbinu za upili. Mbinu ya msingi iliyotumika ni mbinu ya usomaji makini na mbinu ya upili iliyotumika ni upitiyaji wa nyaraka.

3.5.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Usomaji makini wakati mwengine hujulikana kwa jina la usomaji wa kina. Kwa mujibu wa Robson (2000) anasema kuwa hii ni mbinu ya utafiti inayomtaka mtafiti kusoma kazi alizoziteuwa kwa makini ili aweze kupata data anazozikusudia zijibu maswali yake ya utafiti. Ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka katika matini zilizoteuliwa katika utafiti husika. Kupitia mbinu hii mtafiti huteuwa matini maalum, huzisoma matini hizo kwa kina huku akikusanya data zinazohusiana na utafiti wake. Tunasema ni mbinu ya usomaji makini kwa sababu mtafiti huzisoma kazi hizo tena na tena, mpaka pale anapojiridhisha kuwa sasa amepata data anazozihitaji.

Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kwa kupitia mbinu ya usomaji makini kutoka katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Mtafiti aliandaa daftari maalum ambalo aliligawa katika sehemu kuu tatu na kila sehemu ikiwa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengo mahsusi ya utafiti wake. Hii ilirahisisha kukusanya data kutoka katika tenzi teule zinazohusiana na malengo yetu mahsusi.

3.5.2 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka

Kwa mujibu wa Hucker (2001) nyaraka ni kitu chochote kilichoandikwa au kuchapishwa ambacho humsaidia mtafiti kupata data za utafiti wake. Nyaraka zilizopitiwa katika utafiti huu ni vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali yenye mada zinazofanana na utafiti wetu, katika maktaba zilizoteuliwa. Nyaraka hizi zilisaidia kushadidia na kukazia maarifa katika data za msingi.

3.6 Uteuzi wa Watafitiwa

Enon (1998) anasema kuwa uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuchaguwa au kupata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Katika utafiti huu mtafiti ametumia uteuzi lengwa.

3.7 Uteuzi Lengwa

Enon (ameshatajwa) anasema kuwa uteuzi lengwa ni ule uteuzi ambao mtafiti huenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data atakazozihitaji ili kupata data za utafiti wake. Mtafiti amezichaguwa kazi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* akiamini zimesawiri vyema mila na desturi za mwanamke wa visiwani. Hivyo mtafiti aliamini kuwa kazi hizo zitatowa picha za uhalisia wa kile kinachotafitiwa.

Vilevile kazi hizi teule ziliateuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi lengwa kwa sababu mtafiti ameamini kuwa kazi hizo zitampatia data zinazohitajika. Babbie, (1999) anaeleza kuwa uteuzi wa watafitiwa lengwa ni mbinu ya uteuzi wa wateuliwa wa utafiti ambao mtafiti huteuwa watafitiwa fulani akiamini kuwa watafitiwa hao ni sahihi. Sampuli lengwa inayo manufaa makubwa kwa mtafiti

kwani humuwezesha kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Hii ni kwa sababu mtafiti hatumii muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki.

3.8 Watafitiwa

Ni watu au vitu walioteuliwa au vilivyoteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi husika. Kothari (1990). Hivyo utafiti huu umechunguza vipengele vinavyohusiana na mila na desturi za mwanamke wa visiwani vinavyojitokeza katika tenzi teule. Kazi hizo zilichaguliwa kutokana na kutofanyiwa utafiti wa kina katika vipengele vya mila na desturi za mwanamke wa visiwani.

3.9 Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kipengele muhimu sana katika kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanapatikana na hivyo utafiti nzima kukamilika. Katika utafiti huu tumetumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika kuchambuwa na kuwasilisha data. Kothari (ameshatajwa) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambuwa data, ambapo mtafiti huzichambuwa data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mbinu hii hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi, kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno, aidha ya kuandikwa au ya kuzungumzwa.

3.10 Hitimisho

Sura hii ya tatu imeelezeya mambo ambayo yana msingi sana katika kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Katika kufanya utafiti

wetu,kukamilika na kuaminiwa tumekusanya data za msingi na data za upilikwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka maktabani na usomaji makini katika tenzi zilizoteuliwa. Data za upili zimetumika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi. Pamoja na hayo, sehemu hii ilielezea watafiti wetu, watafitiwa, eneo la utafiti, umbo la utafiti na usampulishaji lengwa. Sura ya nne inazungumzia uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti pamoja na mbinu za kifani zilizoibuwa mila na desturi zimetolewa uafafanuzi wake.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kutathmini mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Kwa ujumla sura hii imejaribu kuwasilisha na kuchambuwa data za utafiti zinazohusiana na malengo mahsusi matatu ambayo ni : kuainisha mila na desturi zinazojitokeza katika tenzi teule, kuchunguza mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazopatikana katika tenzi teule na kubainisha mbinu za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*.

Sura hii ina sehemu kuu nne, sehemu ya kwanza, inahusu muhtasari wa kitabu teule pamoja na usuli wa mwandishi. Sehemu ya pili inazungumzia uainishaji wa mila na desturi zinazojitokeza katika tenzi teule, sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa data za mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazopatikana katika tenzi teule. Na sehemu ya nne inaeleza ubainishaji wa mbinu za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*.

4.2 Muhtasari wa Kitabu Teule

Diwani hii ya *Howani Mwana Howani* ni Diwani ambayo imekusanya tenzi mbili (*Howani* na *Mwana Kukuwa*) ambazo zinasimulia ada, mila, desturi, pamoja

na mafunzo ya dini na dunia yanayoambatana na vipindi mbalimbali vya maisha ya mwanamke wa visiwani (Zanzibar), kuanzia kuzaliwa kwake, utoto wake, avunjapo ungo na kuwa mwari, anapoposwa, kufungishwa ndoa na kuolewa, maisha ya ndoa na ulezi wa mimba.

Huo ni utamaduni ambao unamuongoza mwanamke na kumfungamanisha na maadili ya jamii yake. Ada, mila na ngoma zake pekee ambazo kila kukicha zimo katika hatari ya kumezwa na kugubikwa na utamaduni wa kigeni. Mwandishi amejaribu kuyahifadhi haya kwa beti zenye kudhihirisha ukwasi mkubwa wa lugha na umahiri wa utunzi.

4.2.1 Usuli wa Mwandishi

Bi. Zaynab Himid Mohamed alizaliwa tarehe 12 Februari 1918 mtaa wa Malindi, na alianza shule tareha 01 Juni 1921 huko Forodhani. Akiwa miongoni mwa wasichana wachache wa Kiafrika kusoma shule huko Zanzibar. Mwaka 1934, Bi. Zaynab alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi waliofaulu na kupata nafasi ya mpango wa “pupil teacher” yaani mwalimu mwanafunzi

Mwaka 1936 mwezi wa kwanza alianza kazi ya ualimu katika shule ya “Town Primary” mjini Unguja akiwa na wanafunzi 16. Bi. Zaynab aliolewa na mtoto wa shangazi yake mwaka 1936 mwezi wa kumi na mbili akiwa na umri wa miaka 18. Mwaka 1938 alipata uhamisho wa kikazi na kwenda kusomesha Pemba, na aliamuwa kwenda huko pamoja na pingamizi ya mume wake. Huko alifanywa mwalimu mkuu wa shule ya Chachani. Baada ya hapo alisomesha shule mbalimbali za Unguja na Pemba.

Bi. Zaynab alipata nafasi za kuwaongoza wenzake kwa kufanya safari za mwanzo za kiserikali kwa mwanamke kwa kutembea Uingereza 1960, ambako alijifundisha mambo mengi ya uendeshaji shule. Vilevile Bi. Zaynab alisafiri katika nchi mbalimbali kama vile: Paris, Misri, Lebanon, Syria, Esrael, Iraq katika mwaka 1962. Bi. Zaynab alijituma sana katika sekta ya elimu kwa kuweka nidhamu na mipaka mizuri mpaka akatunukiwa nishani ya daraja la pili ya “brilliant star” na Mfalme Abdalla bin Khalifa mwaka 1963, alikuwa ni mwanamke wa kwanza kupata nishani katika idara ya elimu.

Bi. Zaynab alipata uzoefu wa kuandika wakati akiwa mwalimu. Alipewa kazi na mzee A.A. Karume, muda mfupi baada ya mapinduzi ya Januari 1964, kuandika mchezo wa kuigiza kwa jina la “Unguja ya Leo Sio ya Jana”. Pia alitunga shairi la kuusifu muungano lilisomwa na watoto waliokwenda Dar es salaam kutoka Zanzibar katika sherehe za Muungano.

Vilevile alitunga shairi la kumsifu Mwalimu J.K. Nyerere ambalo aliliita “Nyerere Raisi Mwema, Mwenye Busara na Hima”. Shairi jengine la Mwalimu lilisomwa Dar es salaam tarehe 10 Oktoba 1965, wakati wa sherehe za miaka mitano tokea Nyerere kuwa Raisi.

Pia alitunga shairi la kusomwa mashuleni kila asubuhi, akisaidiwa na Seif Salim na Idd Farhan, wanamuziki na watunzi mashuhuri wa Zanzibar. Bi. Zaynab aliwahi kuolewa vyuo vitatu, lakini hakubahatika kupata watoto. Mwandishi huyu alifariki tarehe 31 Disemba 2002 ambapo kazi yake hii ilikuwa katika mchakato wa kuchapishwa.

4.3 Kuainisha Mila na Desturi Katika Tenzi za Howani na

Mwanakukuwa

4.3.1 Utangulizi

Lengo la kipengele hiki ni kuainisha mila na desturi zinazojitokeza katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Vigezo vya uainishaji vilivyotumika ni vya kimaudhui. Kwa kutumia kigezo hiki tumezigawa mila na desturi hizo katika vifungu vifuwatavyo: malezi ya mtoto wa kike na kiume, sherehe za jando na unyago, mafunzo/kufunda, mavazi, ngoma za asili, tiba za asili, mapambo ya wanawake wa visiواني, elimu, pamoja na ndowa za visiواني. Mtafiti alizipata mila na desturi hizi kwa kutumia njia ya usomaji makini katika Diwani teule.

4.3.2 Malezi ya Watoto

Mtoto wa kike na wa kiume wa visiواني, wanapozaliwa na kukuwa hufundishwa mambo mbalimbali ambayo huwa ni maadili mema ya kuishi vizuri katika jamii. Mtoto wa kike hufundishwa na akina mama maadili mema ya kuishi na mume vizuri, na namna ya kutunza familia anapoolewa na kuzaa. Mtoto wa kiume hufundishwa na akina baba maadili ya kuishi vizuri na jamii, mke, kufanya kazi kwa bidii ili aweze kujitegemea katika kutunza familia wakati wa kuo utakapowadia.

4.3.3 Sherehe za Jando na Unyago

Jamii ya visiواني pia ilikuwa na sherehe za jando na unyago. Mtoto wa kiume alifanyiwa tohara alipotimia umri wa kuelewa na kupambanua mambo vizuri, huko hufundishwa mambo mbalimbali yanayohusu maisha ya baadae, kama vile: kuishi na jamii vizuri, kuwa mchapakazi n.k.

Ama kwa upande wa mtoto wa kike alipata mafunzo ya unyago mara tu alipovunja ungo. Mwari alifikia umri wa kupewa mafunzo ya unyago pale tu alipovunja ungo kwa kuiona hedhi. Baada ya kuiona hedhi kwa mara ya mwanzo mama humpeleka binti yake kwa somo yake, somo nae hukusanya watu wake na hapo humwalika mwari ndani kwa muda wa siku saba na kumfunza mambo mbalimbali yanayohusu maisha. Mambo anayosisitizwa zaidi ni kufanya kazi kwa bidii, usafi wa mwili na nyumba, mazingira na elimu ya familia. Mafunzo hayo yote hutolewa kwa kupitia nyimbo mbalimbali.

4.3.4 Mafunzo/ Kufunda

Kwa mujibu wa Tuki (2004) mafunzo ni mambo anayofundishwa mtu kwa muda fulani, masomo. Sengo (1991) anaelezea kuhusu mila na tamaduni za jamii ya watu wa pwani, akianza na jando anasema kuwa. Jando ni chuo muhimu sana cha mafunzo ya maisha ya pwani kote. Chuo hiki kinamtoa mtu usungoni na kumtia uromboni. Watoto aghlabu, hupelekwa wakiwa na umri wa kusikia na kushika ili wakitoka huko, warudi wakiamini kuwa wao ni watu wazima. Huko jandoni wari wanatakiwa kuyajuwa mambo ya kiutu uzima. Chuo hiki kwa upande wa wanaume, kinawaeleza masuala yote muhimu yanayohusu jinsia, wanawake, ulezi, pamoja na kuwakomanza wawe wavumilivu na wajuzi wa mambo na hali mbalimbali.

Ama unyago ni Chuo kama jando, lakini kinahusu zaidi wanawake. Nao kama wenzao, huambiwa yote yanayowahusu wanaume, ndoa na namna ya kuyamudu maisha. Fahari ya mrombo wa kike ni kuolewa na kuishi kistahiki maisha yake yote.

4.3.5 Ndoa za Watu wa Visiwani

Ndoa za watu wa visiwani zilifanyika kwa makubaliano kati ya wazazi wa mtoto wa kiume na mtoto wa kike. Kwa kawaida mahari yaliyotolewa yalikuwa ni makubaliano baina ya wazazi wa pande zote mbili. Baada ya kukubalika kwa mahari wazazi wa pande zote mbili hukutana kwa lengo la kupanga siku ya harusi. Siku hiyo hutazamwa kwa mganga au mnajimu ili kuepusha balaa au husda za watu wabaya.

4.3.6 Elimu

Wazee wa zamani wa visiwani, hawakupenda kuwasomesha watoto wao shuleni, wakiamini kuwa wakipata elimu wataingia katika ukafiri au watakojowa usimama. Elimu iliyotolewa kwa watoto wa visiwani ilikuwa ni elimu ya Madrasa. Mtoto alipotimia umri wa miaka mitano hadi sita, alipelekwa Chuoni kwa lengo la kumfundishwa Qur-ani ili amjuwe Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

4.3.7 Ngoma za Asili

Ngoma za asili za visiwani ni lelemama, msondo, msewe beni, taarabu, bomu, boso, n.k. na ambazo baadhi yake zinaendelea hadi sasa. Ngoma hizo huchezwa kwenye sherehe mbalimbali pamoja na shughuli mabilimbali za kitaifa, kama vile, sherehe za harusi, sherehe za jando na unyago, shughuli za kisiasa n.k. Baadhi ya ngoma hizo kwa sasa ni nadra kuzisikia, hii ni kutokana na wapigaji na wachezaji wa ngoma hizo kuwa wazee sana na wengine wameshafariki.

4.3.8 Tiba za Asili

Watu wa visiwani walitumia na hadi sasa wanatumia mizizi, majani, tunda za mimea, mafuta ya nazi au ya halizeti yaliyochanganywa na dawa nyengine kama tiba ya magonjwa mbalimbali yanayowasumbuwa, ambazo walizisaga au walizichemsha. Dawa za kunywa zilimsaidia mgonjwa kuondoa maradhi yaliyo mwilini mwake na dawa za kufukiza zilitumika kwa lengo la kufukuza mashetani wabaya.

4.3.9 Mapambo/Urembo wa wanawake wa Visiwani

Wanawake wa visiwani walitumia mapambo mbalimbali kwa ajili ya kuiremba miili yao. Miongoni mwa mapambo waliyoyatumia ni vidani, vipini, vikuku vya mikononi na miguuni, bangili hereni n.k, mapambo hayo yalikuwa ya dhahabu, fedha au kareti. Wanawake hawa walitumia manukato mbalimbali ya kufukiza, kujipaka na kuvaa, miongoni mwa manukato hayo ni : asumuni, vilua, nargisi, mhanuni, mawardi, udi na ambari, hal-udi, vikuba, marashi, tunda za marijani n.k. Vilevile walijitona kwa hina miguuni na mikononi, na machoni walijiremba kwa wanja.

4.3.10 Mavazi ya Watu wa Visiwani

Kwa upande wa wanaume walivaa seruni, kanzu, joho, kilemba na makubadhi wakati walipokwenda kuoa. Mavazi mengine ya wanaume ni baraghashia, suruali na shati, soksi nakadhalika. Ama kwa upande wa wanawake walivalishwa kanga za kisutu wakati wanapoolewa. Mavazi mengine ya wanawake ni buibui la kizoro, kanga mbili, kanzu, mtandio, hafu, kilemba, ukaya, kigwe, melimeli, sapatu, nakadhalika. Lengo hili limetowa mwanga

mkubwa katika kukamilisha malengo mengine. Hii ni kwa sababu, tumepata maelezo kamili yanayohusiana na vipengele mbalimbali vinavyohusu mila na desturi za mwanamke wa visiwani katika tenzi husika na khatimae kuvifanyia kazi kwa ajili ya uchambuzi.

4.4 Uchambuzi Wa Data za Mila na Desturi Katika Tenzi Teule

4.4.1 Utangulizi

Mila na desturi za mwanamke katika kazi za fasihi zimefanyiwa kazi na wahakiki mbalimbali pamoja na watunzi mbalimbali wa kazi za fasihi za ushairi, riwaya, tamtiliya, nyimbo, ngano n.k. Mila na desturi hizo hujitokeza katika namna mbalimbali ambazo zinaweza kufaa na nyengine hazifai. Mathalan, kuna baadhi ya mila na desturi kama vile kupigana vijembe, kuvaliana kanga zilizoandikwa mafumbo, kupeana majini, kurogana, na nyenginezo, ni baadhi ya mila na desturi ambazo hazifai kuendelezwa katika jamii yoyote ile duniani.

Katika sehemu hii, tumefanya uchambuzi wa data mbalimbali zilizokusanywa na mtafiti katika tenzi teule, ambazo ni mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani. Mila na desturi hizo zimechambuliwa katika vipengele vifuwatavyo : ulezi wa mimba na kujifunguwa, malezi ya mtoto wa kike, elimu, sherehe za unyago, mafunzo, ndoa za wanawake wa visiwani, ngoma za asili, tiba za asili, mapambo, pamoja na mavazi ya wanawake wa visiwani.

4.4.2 Uchambuzi wa Mila na Desturi Katika Utenzi wa Howani

4.4.2.1 Malezi ya Mimba na Kujifunguwa

Mdee na wenzake (2011) wanasema kuwa, malezi ni namna ya kumlea mtu au mtoto kwa mujibu wa taratibu zilizokubalika, makuzi, ulezi, lisha, uangalizi. Nao BAKIZA (2010) wanasema, malezi ni makuzi ya mtoto kufuatana na utamaduni wa jamii. Tunaziunga mkono maana hizo hapo juu kwa kusema, malezi ya mimba ni namna ya kumlea mtu ambae amebeba ujauzito kwa mujibu wa taratibu au mila na desturi zilizowekwa na jamii husika.

Uzazi ni kielelezo cha kuwepo na kukuwa kwa jamii ya mwanadamu popote pale ulimwenguni. Iwapokuwa uzazi ni kitambulisho kikubwa cha kuwepo (uhai) na kukuwa kwa jamii, mtazamo juu ya jambo hili kwa jamii moja au nyengine unaweza kufanana au kutofautiana kulingana na mazingira ya jamii. Kileo (2011). Katika antolojia ya kibantu, uzazi huchukuliwa kama kitu muhimu sana katika asili ya Wabantu na kinachoweza kuleta mshikamano katika ndoa na ndani ya familia.

Kwa Wabantu uzazi ni suala zito na linaheshimiwa na kuthaminiwa katika jamii zao. Katika jamii za Wabantu kuna sherehe mbalimbali zinazofanywa ambazo lengo na madhumuni yake ni kuenzi uzazi. Kwa mfano sherehe za kuzaliwa na kumpa mtoto jina zinaashiria kusherehekea kuongezeka kwa ukoo. Hivyo wanajamii wanasherehekea kwa lengo la kumkaribisha mwanafamilia mpya katika jamii Mbiti akinukuliwa na Kileo (2011).

Kwa mila na desturi za wanawake wa visiwani hapo kale, malezi ya mimba yalianza mara tu mwanamke alipobeba ujauzito. Mtoto wa kike anapoolewa na kubeba ujauzito alikuwa hapelekwi hospitali, kwa vile huduma za hospitali zilikuwa hakuna. Zaidi walikuwa wanawatumia wazee ambao walikuwa na elimu ya kujuwa mambo mbalimbali yanayohusiana na wanawake na watoto. Bi Zaynab ameyazungumza haya katika beti za (14, 15 na 22).

Katika beti hizo, mshairi anatueleza kuwa wanawake hao walipobeba ujauzito walikuwa hawajui, na wala hawakujuwa miezi ya ujauzito wao. Hii ilitokana na kutokuweco na madaktari na vyombo vya kitaalamu vya kuwajulisha mambo hayo, badala yake, walimwita bibi mkunga, bibi huyo aidha alikuwa ni bibi katika familia au alikuwa ni jirani wa karibu. Ili kujuwa kwamba mtu ni mjamzito, bibi mkunga alilikanda tumbo la mgonjwa kwa mafuta ya nazi au ya halizeti, kutokana na utaalamu wake alitambuwa kuwa mgonjwa ana ujauzito na alitambua miezi ya ujauzito huo.

Baada ya mgonjwa kutambuwa kwamba ni mjamzito, huulea ujauzito wake kwa kutumia madawa mbalimbali ambayo yalimsiadia mgonjwa kuondosha maumivu katika mwili wake. Katika beti za (13 na 45) msanii anasema:

13. Madawa haya na yale

Yalijaa ungo tele

Wazee wapiga kele

Mwenetu yu taabani.

45. Chemsha teleka dawa

Vijunguni vikitiwa

Mvuje nikatiliwa

Habasoda chetezoni.

Kutokana na beti hizo hapo juu mwandishi anatueleza kuwa, ni mila na desturi za wanawake wa visiwani kuzilea mimba zao kwa kutumia madawa mbalimbali. Walifanya hivyo kwa lengo la kuuchangamsha mwili wa mjamzito na kumkinga na mashetani wabaya ambao wanaweza kuhatarisha maisha yake na maisha ya kiumbe kilichomo tumboni. Dawa za kunywa zilimsaidia mjamzito kuondosha maumivu katika mwili wake, na dawa za kufukiza kama vile habasoda, mvuje na nyenginezo, zilitumika kama kinga ya mashetani wabaya.

Mama mjamzito alipofikia miezi saba alialikwa ndani na hakuruhusiwa kutoka nje mpaka wakati wa kujifunguwa ulipofika. Mila na desturi hii ilifanywa kwa lengo la kumkinga mjamzito na vijicho pamoja na midomo ya watu. Mambo yote hayo yalifanyika kwa sababu, katika jamii kuna baadhi ya watu aidha wanawake au wanaume, wanapotazama au kusema basi macho na midomo yao huweza kuleta madhara kwa mjamzito au mtoto mchanga. Mimba ilipofikia miezi tisa na siku ya kujifunguwa, bibi mkunga hakutoka katika chumba cha mjamzito kwa lengo la kumpokea.

Vilevile baadhi ya majirani walijikusanya ukumbini ili kupiga kelele. Haya yote tunayapata katika beti za (47, 48, 49, na 52) wakati mama Sihadaike anapomsimulia mwanawe mambo hayo. Wazee hawa wa kale walipiga kelele wakati mzazi anapopiga kelele wakati wa kujifunguwa. Mila na desturi hii ilifanywa kwa makusudi ili kuweza kuzizuia kelele za mjamzito anaejifunguwa zisienee mtaani. Hii ni kwa sababu wakati wa kujifunguwa ni wakati nzuri

sana unaotumiwa na mahasidi kuwahusudi watoto wa wenzao kwa kuwatowa kafara.

Baada ya kujifunguwa, mzazi aliamia kwenye kitanda cha kamba kwa ajili ya kuota moto, beti za (75 – 78). Mwanamke yoyote hapo kale na hadi sasa, baada ya kujifunguwa huwekwa kwenye kitanda cha kamba kilichotandikwa mkeka, chini ya kitanda huwekwa gae la moto na kuanza kuuota moto huo ili aweze kurudisha uzima wake alioupoteza wakati wa kujifunguwa. Hapo hufukizwa madawa mbalimbali kwa lengo la kufukuza mashetani wabaya.

Ni kawaida ya mzazi wa kale na hivi sasa kuoga kwa maji ya moto na baadae kukandwa kwa majani ya mbono (mbarika), haya tunayapata katika beti za (79 – 85). Beti hizo zinatueleza kuwa baada ya mzazi kukandwa kwa majani ya mbono, husuguliwa kwa mafuta ya halizeti kwa sababu ndiyo yanayokazanisha mwili. Baadae hulazimika kunywa uji wa mtama ambao umechanganywa na vishuo mbalimbali kama vile: pilipili manga, bizari nzima, mdalasini, siki ya zabibu n.k. Viungo hivyo hutiwa makusudi ili kukamua uchafu uliomo kwenye tumbo la mzazi na aweze kurudi hali yake kwa haraka. Mzazi huyo hukaa ndani kwa muda wa siku arubaini, ndipo hutiwa tohara na shekhe aliyeaminika na baadae hutoka nje.

Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia, mila na desturi hizi za mwanamke wa visiواني katika kipindi cha ulezi wa mimba na kujifunguwa, ni mila na desturi ambazo zinahusiana moja kwa moja na mazingira ya mwanadamu katika jamii husika. Mila na desturi hizi ni vitu ambavyo vimehibitiwa katika

jamii kupitia nyanja za maisha hususan katika wakati na mahali. Maherey (1978) na Eaggleton (1983).

4.4.2.2 Malezi ya Mtoto wa Kike

Kwa muijibu wa Mdee (ameshatajwa) malezi ni namna ya kumlea mtu au mtoto kwa mujibu wa taratibu zilizokubalika katika makuzi, ulezi, lisha, uangalizi n.k. Nao TUKI (2004) malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuwata tabia na mwenendo unaostahiki, makuzi, funza n.k. Tunakubaliana na maoni haya na kufafanua zaidi kuwa, malezi ni namna ya kipekee ya kumlea mtu au mtoto, huku akitarajiwa kuwa atafuwata tabia na mwenendo unaokubalika katika jamii. Kulingana na madai haya, asielelewa kwa namna ya kufuata taratibu zilizokubalika katika jamii husika hutazamwa kama mkiuka maadili kwani atakuwa na tabia zinazokiuka maadili katika jamii yake. Dini ya kiislamu inatilia mkazo umuhimu wa matunzo ya mtoto, na inaonya vikali kuhusu wazazi wanaozembea katika malezi ya watoto wao, kwani haitaki watoto waingie katika maangamizi. Qur-an inasema kuwa, “Wala msijiingize kwa mikono yenu katika maangamizi...” (2 :145).

Mila na desturi katika malezi zimezungumzwa sana katika utenzi wa *Howani*. Uzazi na malezi ni masuala mawili yanayohusiana na ndoa na malezi ya watoto. Mara nyingi katika jamii nyingi za Kiafrika huwa ni jukumu la mwanamke kuwalea watoto wake. Utenzi huu umeonesha kuwa mama ndie aliyepewa jukumu kubwa zaidi katika malezi ya watoto, hususan katika malezi ya mtoto wa kike, kuanzia atakapomzaa mpaka kufikia umri wa

kuolewa. Mama mzazi na mabibi huanza ulezi mara tu mtoto anapozaliwa kwa kumfanyia mambo mbalimbali ambayo ni mila na desturi zao. Miongoni mwa mila na desturi zinazofanywa katika malezi ya mtoto ni hizi zifuwatazo:

Baada ya mtoto kuzaliwa alisafishwa vizuri na kuvalishwa nguo, baadae alilazwa kwenye ungo uliotandikwa kanga kama ni kigodoro cha kulalia na mto wake ulikua ni mchanga, beti za (59 – 62). Katika utenzi huu tunamuona mama Kukuwa akimsimulia mtoto wake jinsi alivyolazwa kwenye ungo. Lengo kubwa la kuwekewa mto wa mchanga ndani ya ungo ni kutengeneza kisogo cha mtoto ili kiwe sawa. Wakati huo mtoto hufungwa dawa mikononi mwake kama vile mvuje, ambao huchanganywa na chumvi ndani yake. Ndani ya ungo aliolazwa mtoto, ilikuwa ni mila na desturi kuwekwa kaa la moto, kiwembe, chumvi na ndimu, wazee hao waliviweka vitu hivyo ili kumkinga mtoto na majini ya subiani, Bi Zaynab anamsimulia mwanawe katika beti za (68, -70, 141).

Inapofikia muda wa siku arobaini, kwa mila na desturi za wanawake wa visiwani hapo zamani, mzazi na mtoto wake walitolewa nje kwa furaha na vicheko na hapo ndipo mtoto anapopewa jina. Bi Zaynab ameyazungumza haya katika beti za (89, 92, 96, 97, 98, 103, 104, 105). Siku ya arobaini wazazi huwa na sherehe ya kumtoa nje mzazi na mjukuu wao. Baada ya kutolewa nje mtoto hupewa jina. Hapo zamani mtoto hakupewa jina tu kama tunavyofanya hivi sasa, bali majina ya mtoto yaliandikwa kwenye vikaratasi saba na kuchaguliwa kikaratasi kimoja ambacho kinakuwa na jina la mtoto. Mtu ambae alipewa uhuru wa kuchagua jina katika vikaratasi hivyo, alikuwa ni

bibi wa baba au wa mama. Bibi huyo huchaguwa kikaratasi kimoja kati ya hivyo saba na kukifunguwa baadae hulitamka hadharani jina la mjukuu wake ili waliohudhuria walitambuwe jina la mtoto huyo. Baada ya hapo mzazi na mtoto wake huweko huru kutoka nje. Msanii anatueleza mila hizo ambazo alifanyiwa Kukuwa katika beti hizo hapo juu.

Watoto wa visiواني hapo kale na hadi sasa, walipakwa wanja machoni na usoni ili wasionekane sura zao. Mwandishi ametueleza haya katika beti za (128 -131, 138). Pale ambapo alikuwa akimsimulia mtoto wake. Mtoto wa kike alipakwa wanja machoni ili atakapokuwa mkubwa awe na haya usoni. Dhumuni jengine la watoto kupakwa wanja lilikuwa ni kuficha sura yake halisi ili aepukane na uhasidi wa mdomo na kijicho. Katika beti za (128, 130, 131 na 138) msanii anasema.

128. Akapakwa mwingi muru

Apate kuwa na nuru

Litokuja haidhuru

Lipae huko mbinguni.

131. Pia apunguze jicho

Uhasidi huwa macho

Kumuona alo nacho

Akaumiya moyoni.

130. Itikadi ilikuwa

Machoni huu kutiwa

Mwanamke tapokuwa

Awe na haya usoni.

138. Usiku pia mchana

Akirembwa sanasana

Usoni hukimuona

Mila hii ya zamini.

Mila na desturi nyengine ambayo ilifanywa na wanawake wa visiواني katika malezi ya watoto wao, ilikuwa ni kuzipazisha sauti zao kwa kumbembeleza

mtoto wakati anapolia usiku. Mila na desturi hii ilifanywa kwa lengo la kuificha sauti ya mtoto mchanga anaelia isisikike nje, ili asije akadhurika kwa kuchombezwa na masheteni wabaya wa usiku huko nje. Haya tunayapata katika beti ya (140).

Watoto wa visiwani walipotimia umri wa miaka mitano hadi saba walipelekwa Chuoni kwa ajili ya kufundishwa kuisoma Qur-ani. Kipindi hiki nacho huwa kina mila na desturi zake, beti za (158 na 159, 164, 166, 174, 183 na 184, 186 na 188). Katika beti hizo msanii anatueleza kuwa, Sihadaike alipotimia umri wa kupelekwa Chuoni, alipelekwa ili kwenda kuisoma Qur-an. Kwa mila na desturi za wanawake wa visiwani hapo zamani, mtoto alipelekwa chuoni na ufito kama ni fidia kwa mwalimu wake. Vilevile mtoto alitakiwa aende na ubao uliopakwa rangi nyeusi ili utumike kwa kufundishwa kuandika hati za Qur-ani zilizomo kwenye juzuu, kama tunavyomuona Kukuwa.

Baada ya mtoto kuhitimu Qur-ani, wazazi wa mtoto hupeleka sadaka msikitini, huko huombewa dua mbalimbali ili akulie katika misingi ya kuifuwata vyema dini yake ya kiisilamu, kama walivyofanya wazazi wake Kukuwa. Katika beti za (188 na 190) Msanii anasema,

188. Palipelekwa kidogo

Ni sadaka ndogondogo

Kupelekewa vigogo

Vilivyo msikitini.

190. Wakaziomba na dua

Bila hata kuchelewa

Kumuomba mwenye quwa

Rabbil-Alamini.

Baada ya kuhitimu kuisoma vyema Qur-ani, mtoto wa kike alibakia nyumbani na kufundishwa mambo mbalimbali na mama yake yakiwemo mafunzo ya dini ambayo kwa hapa ni dini ya Kiislamu, haya tunayapata katika beti za (191, 192, 193- 233. 256- 259, 262- 264).

Katika utenzi wa *Howani* Bi. Zaynab amemtumia mama Kukuwa ambae alimlea mtoto wake katika maadili ya Kiislamu, kwa kumfunza nguzo tano za Kiislamu, beti za (191, 193-233). Pia alimuusia kuacha mambo ambayo dini yao imeyakataza, kama vile kuepuka hasada na maovu, kuepuka wizi n.k. katika beti za (325- 327). Vilevile mama huyu alimfundiahsha mtoto wake kazi za mikono ambazo zitamsaidia kuyamudu maisha wakati atakapokuwa kwake, na kuacha utegemezi kwa mume wake. Katika ubeti wa (266) msanii anasema,

266. Haya utapoolewa

Kichwani utachukuwa

Pengine utachopewa

Hakikutoshi jikoni.

Miongoni mwa kazi za mikono ambazo mama Kukuwa alimfundisha mtoto wake ni: kusuka ukili (257), kushona makawa, misala na mikeka (258), kushona charahani (262), kutengeneza nakshi za kila aina (259), na kusuka nywele katika mitindo mbalimbali (263 na 264).

4.4.2.3 Masuala ya Elimu

Kwa mujibu wa BAKIZA, (2010) elimu ni maarifa anayoyapata mtu baada ya kujifunza jambo, ujuzi. Kuhusu masuala ya elimu wanawake wa visiwani hawakuwapeleka watoto wao shuleni wakiamini kuwa wakipata elimu ya shule wataingia katika ukafiri au watakojowa usimama. Elimu iliyotolewa kwa watoto hawa ilikuwa ni elimu ya dini yao ya Kiislamu. Kwa mtoto wa kike hakisomesywa shule ikiaminika kuwa atanufaisha kule ambako ataolewa.

Dini ni mfumo maalum wa maisha alioridhia Mwenyezi Mungu kwa waja wake, nao ni sheria na hukumu zilizomo katika Qur-an Tukufu na ubainifu wake katika ulimi wa bwana Mtume Muhammad. Sameja (2002). TUKI (2004) wanafafanua Dini kama imani inayohusiana na mambo ya kiroho, kwamba kuna muumba aliyeumba ulimwengu huu, na kwamba ndie mtawala wa kila kitu kilichomo ndani yake. Pia ni mfumo fulani wa imani na njia ya kuabudu, kusali au kumtii huyo muumba, kama vile Uislamu, Ukristo na Ubudha.

Tunakubaliana na maoni haya na kufafanua kuwa, dini ni uhusiano wa kiroho unaohusu imani kubwa baina ya wanadamu na Mungu. Imani ya kidini inashikilia kuwa Mungu aliumba ulimwengu na hata binaadamu, ambae hata baada kufa, inaaminika kuwa roho yake itaishi mpaka kufufuliwa tena siku ya kiamaa. Katika utenzi wa *Howani* mamaake Sihadaike alianza kumfunza mtoto wake elimu ya Madrasa kwa kumpeleka Chuoni mara tu alipofikia umri wa miaka sita, katika beti za (157 na 158) msanii anasema,

157. *Akakuwa kwa haraka*

Myaka sita akafika

Huku tunahangaika

Sijui tufanye nini.

158. *Sihadaike kakuwa*

Chuoni akatambuwa

Alifu akaijuwa

Kaendelea usoni.

Baada ya Sihadaike kuhitimu Chuoni alibakia nyumbani, mama yake hakumuacha tu burebure, bali aliendelea kumfunza mafunzo mbalimbali yanoyohusu dini yake, katika ubeti wa (191) msanii anasema,

191. *Sihadaike kakaa*

Nyumbani bila hadaa

Na miye sikusangaa

Nikamfundisha dini.

Suwala hili la wazazi wa kike kuwafunza watoto wao dini yoa, tunalikuta katika utenzi wa *Mwanakupona*, pale alipomuusiya mtoto wake *Mwana Hashima* kuzingatia mafunzo ya dini ya Kiislamu. *Mwanakupona* alimuusiya mwanawe juu ya kumtii Mungu na Mtume wake, kupenda na kutenda haki kama dini inavyoagiza, kuswali swala tano za faradhi, kutekeleza sunna n.k. *Mwanakupona* ameyazungumza haya katika beti za (12, 22, na 23). Mulokozi (1999).

Tukirejea katika utenzi wa *Howani* tunamuona mama yake Sihadaike akimfunza mtoto wake dini yao kwa kumfunza nguzo tano za kiislamu ambazo ni: shahada na kumuamini Mtume Muhammad (193 na 195), kuswali swala tano (196 na 197), kutoa zaka kwa yule mwenye uwezo (199 na 200),

kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa yule aliyebaleghe (201 na 202), na mwisho ni kwenda kuhiji Makka kwa mtu ambae anao uwezo wa kihali na mali ya halali (204 na 206). Mama huyu alimfunza mwanawe nguzo hizi ili azifahamu na azifuwate kwa kuzitekeleza ili aepukane na adhabu ya Mwenyezi Mungu kesho kiamama.

Katika kulikamilisha lengo hili la kuwapatia watoto elimu ya dini, mama Sihadaike hakuishia hapo bali alimuusia mtoto wake juu ya kuacha mambo yote ambayo dini yao imeyakataza, na kuyafuwata yote yaliyoamrisha ili apate salama kesho mbele ya Mungu. Mambo ambayo mama Sihadaike alimuusia mwanawe kuyaacha ni: kuepuka hasada na maovu (325 – 327), kuepuka fitna (331 – 333).

Kujiepusha na wizi, zinaa na ulevi (343, 349, 359). Vilevile alimuusiya juu ya kufanya mema (316), kuunganisha udugu (374 na 375), pamoja na kuwatii wazazi hususan baba na mama ili aweze kupata pepo, kwani pepo iko chini ya nyayo za wazazi wawili (baba na mama) (376 -379).

Hivyo elimu hiyo ya dini wazee wa visiwania waliyowafundisha watoto wao, ni miongoni mwa mila na desturi zao, walifanya hivyo ili watoto wao wakulie katika maadili ya dini yao. Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia tunaona kuwa, mambo hayo ya kuwafunza watoto dini yao ni mambo ambayo yamefungamana na jamii yao katika vipindi mbalimbali ambavyo anapitia mwanadamu katika jamii yake kwa ujumla.

4.4.2.4 Sherehe za Unyango

Wanawake wa visiwani pia walikuwa na sherehe za unyago kwa watoto wao wa kike. Mtoto mwari alipelekwa unyagoni mara tu alipovunja ungo. Baada ya mtoto kuvunja ungo alipelekwa kwa somo yake ili apate kufunzwa mambo mbalimbali yanayohusu maisha.

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) wanasema kuwa kuvunja ungo (kubaleghe) ni kitendo cha mtu kutimia umri wa kuweza kuzaa. Tunakubaliana na maoni hayo na kufafanua kuwa, kuvunja ungo ni kipindi ambacho mtoto wa kike anatoka katika hali ya utoto na kuingia katika hali ya utuuzima, kiasi ambacho mtoto huyo inamuhallalikia kufanya maamrishi yote ya Mwenyezi Mungu na kuacha makatazo yake. Kipindi hiki ni kipindi ambacho mtoto anaweza kubeba ujauzito wakati wowote endapo atafanya tendo la ndowa bila ya kujali kuwa ameolewa au hajaolewa.

Katika utenzi wa *Howani*, mara tu Sihadaike alipovunja ungo mama yake alimpeleka kwa somo yake kwa lengo la kumfundisha mambo mbalimbali kuhusu maisha ya baadae. Somo nae alimfundisha Sihadaike mambo mbalimbali kama vile heshima na tohara ili aweze kuondosha uchafu wa hedhi, msanii ameyazungumza haya katika beti za (235 -244). Sihadaike alipotimiza hedhi yake kwa mara ya tatu, somo yake alimpeleka unyagoni. Huko somo na kikundi chake walimfunza Sihadaike mambo yanayohusiana na maisha ya baadae. Nae aliyashika na kuyajuwa mambo yote aliyofunzwa unyagoni. Mafunzo yote yaliyotolewa huko yalitolewa kwa nyimbo mbalimbali zilizosindikizwa na ngoma. Haya yote tunayapata katika beti za (245 -255).

4.4.3 Uchambuzi wa Mila na Desturi Katika Utenzi wa Mwana Kukuwa

4.4.3.1 Sherehe za Unyago

Kama tulivyokwishaeleza katika utenzi wa *Howani* ya kwamba mwari wa visiwanai alipovunja ungo alipelekwa kwa somo ili amfunze mambo mbalimbali kuhusu maisha. Bi. Zaynab ameendeleza sherehe za unyago katika utenzi wake wa pili ambao ni utenzi wa *Mwana Kukuwa*. Katika beti za (09 -25), mwandishi anatueleza kuwa baada ya Kukuwa kuvunja ungo, mama yake alimpeleka kwa somo kwa ajili ya kucheza ili asiwe msungu. Mila na desturi za wanawake hawa waliwaalika watoto wao kwenye unyago kwa muda wa siku saba. Walipowapeleka watoto hao unyagoni waliwapeleka na mkeka, sabuni, birika na peya mbili za kanga kwa ajili ya kumfunga mwari. Wari wanapokuwa unyagoni hufunzwa mambo mengi ambayo yanahusiana na maisha ya ndoa.

Miongoni mwa mambo aliyofundishwa Kukuwa alipokuwa unyagoni ni kuwa mmaridadi (17), kuwa na heshima (18), kuwa mrembo (19) n.k. Kukuwa alikaa huko kwa muda wa siku saba ndipo aliporudishwa nyumbani kwao (21), na hakuyasema mambo aliyofundishwa alipokuwa unyagoni hadi mama yake alipomdadisi kwa kuogopa fedheha na alitosheka na kuamini kweli mtoto wake amefunzwa na kufunzika, mwandishi ameyadhihirisha haya katika beti za (22 – 25).

Baada ya kurudi unyagoni mwari wa visiwanai hapo zamani alibakia nyumbani na kusubiri mume. Wazazi wanapokuwa na mwari ndani ya nyumba huwa na wasiwasi mwingi kwa kukhofia mwari wao asiye akaharibika akiwa

uwarini. Katika utenzi huu msanii anasema kuwa, mara tu Kukuwa aliporudi unyagoni alibakia nyumbani kwa kusubiri mume katika ubeti wa (26 na 36), msanii anasema,

26. *Sasa Kukuwa karudi*

Tukauanza uradi

Dua kaanza shadidi

Kumuombeya mwandani.

36. *Mwali amejaa ndani*

Mungu wangu niauni

Angalau aje nani

Amtoe huku ndani.

Katika beti za (27 – 31) Mama Kukuwa anasema kuwa mzazi anapokuwa na mwari ndani huwa na wasiwasi mwingi, hapo ndipo huanza kazi kubwa kwa mzazi kwani kumlea mwari ni kazi. Anaendelea kusema kuwa, mwari anapokuwa ndani, huwa anampa mzazi wasiwasi na kufikia hatua ya kuighasi nafsi yake kumfikiria mwari wake ni siku gani Mungu atamjalia kupata mume (34 na 36).

Watoto wa kike wa visiwani baada ya kuvunja ungo na kurudi unyagoni walikatazwa kutoka nje. Msanii anayasema haya katika beti ya (32),

32. *Mwanamwali wa zamani*

Hatoki haonekani

Kila saa yumo ndani

Hasikiki abadani.

Mwandishi anatueleza kuwa *Kukuwa* aliporudi unyagoni, hakuruhusiwa kutoka nje na wazazi wake, kiasi ambacho hata palipopigwa hodi nyumbani kwao

kama alikuweco uwani basi alipiga mbio mpaka chumbani kwake ili asionekane na mtu aliyepiga hodi, mila na desturi hii ilifanywa ili kuwaepusha watoto wari kuranda ovyo mabarabarani, na kuwafanya wawe na haya usoni. Msanii ametueleza haya katika beti za (46 -48, na70 – 71). Katika beti za (70 na 71) msanii anasema,

70. Hagongwa wangu mlango

Kwa tumbuo ngo, ngo

Kwa utuo si kishindo

Ni mlango wa uwani.

71. Kukuwa katoka mbio

Kajitanda mtandio

Katupa nazi kizio

Mbuzi ikanguka chini.

4.4.3.2 Ndoa za wanawake wa Visiwani

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamme na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote. Njau na wenzake (2013). Nao Abeid na Olutu (2009) wanasema kuwa ndoa ni muungano baina ya mwanamke na mwanamme. Kwa kawaida huwa ni mkataba wa kihalali baina ya mwanamke na mwanamme ambao hufuwatana na sherehe. Tunayaunga mkono maoni ya wataalamu hapo juu na kufafanua kuwa, ndoa na harusi ni kipengele kinachotafautisha mila na desturi za Waswahili na mila na desturi za makabila mengine. Katika mila na desturi za Waswahili ndoa zinahusishwa na malezi bora ya vijana ambapo ubikira kwa msichana ni kipimo kikubwa cha maadili ya mwanamke anaetarajiwa kuolewa. Kwa mujibu wa mila na desturi za Waswahili maisha ya ndoa ndio kitovu cha maisha ya mwanamke, hivyo anapaswa kuonesha uadilifu na uaminifu kwa muumewe. Msichana anaepoteza

ubikira kabla ya ndoa, huwa mfano mbaya kwa jamii, kwa kuwa kitendo hicho kinadhihirisha kuwa ana tabia mbaya ya kukosa uaminifu, pia ni kukosa heshima kwa wazazi na jamii kwa ujumla. Emmanuel (2015).

Makabila yote ya watu wa pwani, yanashabihiana katika taratibu za kuposa na kufunga ndoa, ambapo wazazi huwa ndio washauri wakubwa wa ndoa za watoto wao na hutumia watu wengine kama mjomba, shangazi na wazee wa mji kufanikisha baadhi ya taratibu za ndoa. Pia Waswahili hutumia watu maarufu kama makungwi na masomo kutoa elimu juu ya maisha ya ndoa kwa vijana wanaotarajia kufunga ndoa. Kwa waumini safi wa dini ya Kiislamu, sheria za kiislamu hutumika kama muhimili mkuu wa kuendesha maisha, kwani dini ndio utaratibu wa maisha ya binaadamu katika kila kipengele cha maisha kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

Katika kuchunguza mila na desturi za mwanamke wa visiwani katika kipengele cha ndoa, tutazigawa katika vipengele vinne ambavyo ni: kipindi cha kutafuta mchumba na kupeleka posa, kipindi cha kupokea mahari, kipindi cha kufungisha ndoa pamoja na kipindi cha baada ya ndoa.

4.4.3.2.1 Kipindi cha Kutafuta Mchumba na Kupeleka Posa

Wanawake wa visiwani walipowatafutia watoto wao wa kiume mchumba, waliwatumia wanawake maarufu mtaani kwa lengo la kufanya upelelezi kwenye nyumba za watu wenye wari, au huoreshana kindugu. Msanii ameyazungumza haya katika beti za (62 – 65). Wakati baba yake muumewe

Kukuwa alipokuwa akimtafutia mchumba mtoto wake, aliwatuma watu wawili kwenda kupeleleza kwao kina Kukuwa. Katika beti za (45, 47, 49 – 61) mwandishi anatuonesha jinsi mpelelezi wa kwanza alipokwenda kwao kina Kukuwa kwa ajili ya kumpeleleza Kukuwa. Vilevile katika beti za (67, 70, 72, 73 -80), mwandishi anatuonesha bi kizee aliyekwenda kwa kina Kukuwa kwa lengo hilohilo la kupeleleza. Mshenga aliyetumwa kwenda kupeleka posa kwao Kukuwa ndie aliyetoa siri ya wapelelezi waliotumwa kwa kina Kukuwa katika beti za (149 -164). Baada ya kuona hayo mama Kukuwa alijuwa kuwa kuna jambo, jambo lenyewe ni kwamba kuna watu ambao wanakuja kumtafutia mtoto wao mke nyumbani kwake. Katika beti za (81 na 82) msanii anasema,

81. Nikawaza haya mambo

82. Huyu ni mtu wa pili

Bila shaka kuna jambo

Kuja kwangu sirisiri

Litaibuka kitambo

Faraji yatukabili

La kheri liko njiani.

Huko siku za usoni.

Baada ya wapelelezi hao kumaliza upelelezi wao, walipeleka habari nzuri kwa baba wa mume (149 -168) na hapo ndipo alipopelekwa mshenga kwa ajili ya kupeleka posa za mtoto wao kwa akina Kukuwa, (136, 139 – 148). Katika beti za (136, 139, 142 na 143) mwandishi anatueleza jinsi mshenga alivyokwenda kwao Kukuwa kwa lengo la kupeleka posa alizotumwa.

Mila na desturi za visiwani pindi mtoto wa kike anapoposwa, baba mzazi hawezi kutoa jawabu la kupokea posa, mpaka familia mbili za kuukeni na kuumeni za mtoto wa kike zikutane na zikubaliane ndipo posa ipokelewe.

Katika utenzi huu, baada ya mshenga kurudi tena kwao Kukuwa ili kusikiliza majibu ya posa aliyotumwa (168 na 169), babaake Kukuwa alisema hawezi kujibu mpaka awaite wazee wa pande zake zote mbili kwa ajili ya kuzungumza, na baada ya kuwafikiana ndipo atakapotowa jawabu kwa mshenga. Msanii anayathibitisha haya katika beti za (170, 171 na 173). Katika beti za (170 na 171) msanii anasema,

170. Alijibu baba mtu

Hakika kwa mila zetu

Kwamba baba hathubutu

Kujibu aseme nini.

171. Shoti kwanza niwaite

Wazee wa pande zote

Tuyazungumze sote

Na posa kuithamini.

Kwa mujibu wa mila na desturi za watu hawa, dini yao ya Kiislamu ilikataza kutangaza posa, bali iliruhusu kutangaza ndoa (harusi), ndio maana babaake Kukuwa akamwambia Mshenga aimezee rohoni posa aliyotumwa katika beti za (172 na 174). Mila na desturi hii ilifanywa ili kuepusha uhasidi wa baadhi ya watu, ambao hawapendelei kheri watoto wa wenzao. Baba Kukuwa anamwambia Mshenga maneno hayo katika beti ya (175) pale aliposema,

175. Kuna watu mahasidi

Hutaka kuyafisidi

Kila linaloshadidi

Kwa kutia nuksani.

Vilevile mwandishi anatueleza kuwa, wazazi wa mtoto anaeposwa hawawezi kupokea posa za mtoto wao mpaka wazichunguze tabia za mtoto wa kiume anaeposewa, pamoja na tabia za wazazi wake. Endapo tabia zao zikikubalika katika familia, ndipo wazazi wa mtoto wa kike humpelekea barua Mshenga kwa lengo la kwenda kuizungumza posa. Katika utenzi wa *Mwana Kukuwa*, wakati mshenga alipokwenda kusikiliza jawabu (193 na 194), babaake Kukuwa alimrudisha (196). Baba huyu alifanya hivyo kwa lengo la kuzichunguza tabia za mtoto wa kiume na familia yake. Baada ya kuyachunguza na kuyapata (207), ndipo alipoandika barua na kumpelekea Mshenga, ili apeleke majibu alikotumwa (210 -212), kwa ajili ya kupokea posa zao.

Baba wa mtoto wa kiume baada ya kupokea barua na kuisoma, alitayarisha watu wake wa kupeleka posa za mtoto wake siku atakapofika, (223 na 224). Babaake Kukuwa nae aliwachaguwa jamaa zake wa karibu ili waje kupokea posa siku na muda utakapofika (229).

Katika beti za (230 -246) wazazi wa pande hizo mbili za mtoto wa kike na kiume, walizungumza posa na babu yake Kukuwa ndie aliyepewa mamlaka ya kutoa jawabu kwa kuzikubali posa zao, lakini wasubiri kwa muda wa miaka miwili ndipo watoe mahari na wapange siku ya harusi. Katika beti za (242 – 245) msanii anasema,

242. *Babu akayatongowa*

Akajibu sawasawa

243. *Kwamba, waheshimiwa*

Miguu mulonyanyuwa

Kwa fasaha na uluwa

Akavuwa na miwani.

Kutafuta hii ndowa

Mimi nimewapokeni.

244. Mikono yetu miwili

Mepokeya jambo hili

Kwa yoyote yetu hali

Sote mekupokeeni.

245. Kaeni mstahamili

Kiasi myaka miwili

Msione kuwa mbali

Inakwenda kama nini.

Baada ya watu kumaliza kupeleka na kupokea posa, mila na desturi za watu hawa walitowa takadumu (sadaka ya chakula), hii ilifanywa kwa lengo la kuwakarimu wageni na kuunganisha udugu ambao hapo awali ulikuwa mbalimbali. Katika utenzi huu, wazazi wa Kukuwa baada ya kumaliza kupokea posa, walitoa dhifa kwa watu waliohudhuria. Msanii ameyazungumziya haya katika beti za (248 na 249).

4.4.3.2.2 Kipindi cha Kupeleka Mahari

Mahari ni mali, kitu au fedha anayotowa mwanamme kumpa mwanamke atakaemuoa. BAKIZA (2010). Mahari ni moja ya mila na desturi za zamani za mahusiano ya kifamilia ya mwanadamu kwamba wakati wa kuoa, mwanamme hulipa mahari kwa mwanamke (atakaemuoa) au kwa baba yake (huyo mwanamke). Na mbali na hilo hutakiwa kujitolea kugharamia gharama zote za mke na watoto katika kipindi cha uhai wake.

Mahari ni moja ya mila na desturi au utamaduni uliotapakaa sehemu kubwa ya sayari hii ya dunia kwa miaka mingi, ambapo watu wengine

wanakubaliana nayo na wengine wakiuponda. Kila jamii ina utaratibu wake wa kutoza mahari, ima iwe kwa taratibu za kidini, kikabila au vyenginevyo, ilimradi lile lengo la kutoa mahari linakuwa limefikiwa na muhusika baada ya kukubaliana na taratibu husika.

Mahari ni aina ya malipo anayolipwa binti au malipo yanayotolewa na upande wa mume anayetaka kuoza kwa wazazi wa binti au bi. Harusi mtarajiwa. Kwa sehemu kubwa malipo haya hutofautiana kati ya kabila moja hadi jengine na kiasi au idadi hutegemea makubaliano baina ya pande mbili husika. Mecey (2011).

Ulipaji wa mahari huwa unategemea jamii waliopo waowaji na huwa haina kiwango maalum. Ndoa katika Uislamu haiwi ila kwa mahari, ni kwa dalili ya neno lake Allah (S.W) katika Qur- an yake tukufu pale aliposema “Na wapeni wanawake mahari yao...” (An-Nisaai :4). Alhidaya.

Uislamu haukuweka kilingo maalum cha kutoa mahari, chochote anachomiliki mtu cha kutoa mahari basi kikubaliwe, wazee wa mtoto wa kike wanatakiwa wasifanye tamaa na kuwachuza watoto wao kwa biashara. Al- kindy (1988). Kwa mila na desturi za visiwani, wazazi wa mtoto wa kike wanapomkubali mume hupeleka habari kwa wazazi wao. Baada ya kuwafikiana, hutoa siku ya kutaja kiasi cha mahari. Baada ya wazazi wa mtoto wa kiume kutajiwa kiasi cha mahari kinachotakiwa, huuliza siku ya kuyapeleka mahari na hapo huambiwa siku ya kuyapeleka mahari hayo. Watu wanaopewa mamlaka ya kufanya hivyo walikuwa ni babu wa baba au mjomba.

Katika utenzi wa *Mwana Kukuwa* baada ya babaake Kukuwa kuzikubali posa za mtoto wake, alipeleka habari kwa wazazi wake na wazazi wa mkewe (260, 261 na 287). Mara tu baada ya kuwafikiana walipeleka mjumbe kwa wazazi wa mtoto wa kiume kujulishwa siku ya kutajwa kiasi cha mahari (312 – 314). Siku iliyopangwa ilipofika, wazazi wa mwanamme waliwapeleka watu wao na kuanza shughuli yao, na hapo walitajiwa siku ya kuyapeleka mahari yao (316 - 327, 337 -341). Aliyeachiwa mamlaka ya kutaja kiasi cha mahari na kutoa siku ya kuyapeleka alikuwa ni babu yake Kukuwa, katika beti za (338 na 339) msanii anasema,

338. *Kashuka matao chini*

Akajibu kwa laini

Mahari tulateeni

Ni rupia elfeni.

339. *Kumi la kwanza shahari*

Mwezi Rabii-l-awali

Ing'arapo kamari

Inapokuwa mbinguni.

Wakati wa kupeleka mahari wanawake hawa hawakuyapeleka kimyakimya kama ilivyo hivi sasa. Mahari yalipelekwa kwa shangwe na nderemo. Somo huwa ndie wa kwanza katika shughuli ya kupokea mahari. Katika utenzi huu, tunaona kuwa wazazi wa mtoto mwanamme waliyatia mahari kwenye khenshe (upatu wa shaba), ambapo waliyapamba kwa kutia asumini na uturi wa aina mbalimbali.

Mahari hayo yalifunikwa kitambaa na alipewa mtoto wa kike aliyevishwa vizuri na kwenda kumkabidhi babu yake Kukuwa, ((353 -359, 459 na 418). Baada ya babu yake Kukuwa kuyapokea mahari, alimkabidhi somo yake

Kukuwa (418). Baada ya mahari ya Kukuwa kupokelewa yalioneshwa kwa watu wote waliohudhuria, baadae watu hao walipewa chakula na kuondoka, (433, 438 -440).

Kufanya harusi si jambo la masikhara la kufanya mtu peke yake, kutokana na gharama nyingi ambazo hutumika kuigharamia harusi. Gharama hizo huanzia kwa bibi harusi, karamu pamoja na vyombo ambavyo hununuliwa bibi harusi kwa ajili ya kwenda kutumia nyumbani kwake. Kwa mila na desturi za wanawake wa visiwani walipokuwa na harurusi waliitana vikao ili kuchangishana michango itakayotumika kwa ajili ya harusi, kama msanii anavyotueleza katika beti za (444, 453, 458, 459, 462, 466, na 468). Imejitokeza pale ambapo wazazi wake Kukuwa walipofanya vikao kwa ajili ya kupeana majukumu ya harusi.

Harusi za wanawake wa visiwani hazikualikwa na mtu mmoja ambae hupita katika nyumba mojamoya na kualika kama tunavyofanya siku hizi. Watu wenye harusi waliwaalika majirani, ndugu na jamaa zao kwa kuviita vyama vya ngoma ambavyo vilipita mitaani na mgoma zao kwa ajili ya kualika harusi. Katika beti za (478 -487, 500). Bibi yake Kukuwa aliomba aitiwe shekhe (mkuu wa kikundi cha ngoma) kwa lengo la kutaka ngoma kwa ajili ya kualika watu ahrusi ya mjukuu wake. Katika beti za (480 na 500) msanii anasema,

480. *Kwamba twataka jaliko*

Na shinda pia iweko

500. *Jaliko kuongozana*

Kwa marefu na mapana

Lelemama takuweko

Furaha kila namna

Nalo bomu uwanjani.

Kualika mitaani.

Nyumba ya kwanza kualikwa harusi ilikuwa ni nyumba ya bwana harusi (503). Kikundi cha ngoma kilichokuwa kikialika harusi kilipofika kwao bwana harusi, shekhe aliwaalika kwa kueleza utaratibu wote ambao utafanyika katika harusi, kuanzia siku ya kuolewa mpaka siku ya kumpeleka nyumbani kwake, (509 – 525). Halikadhalika wazazi wa mtoto wa kiume wanapoalika harusi ya mtoto wao, nao hufanya kama walivyofanya wazazi wa mtoto wa kike, msanii anatueleza haya katika beti ya (528).

4.4.3.2.3 Kipindi cha Kufunga Ndoa

Baada ya wazazi wote wa maharusi watarajiwa kualika harusi, hapo huanza mambo mabalimbali ambayo ni matayarisho ya kuwafungisha ndoa watoto wao. Hapa somo huwa ndie muhusika mkuu wa kumshughulikia Bi. Harusi, kwa kumtayarisha kwa ajili ya ndoa yake. Mambo hayo ni kama vile: kumsinga, kumpaka hina, kumpamba kwa mapambo na manukato mbalimbali.

Jambo la awali ambalo Bi. Harusi hufanyiwa kama ni matayarisho ya ndoa yake ni kusingwa. Kusinga ni kitendo cha kusuguwa mwili kwa kutumia msio BAKIZA (2010). Kusingwa kwa mwanamke kulikuwa na sababu tatu. Mwanamke akisifika kwa mwili laini, mwororo na safi. Hizi zilikuwa ni sifa zikiriwazo sana. Kwa hiyo zile sababu tatu za kusinga zilikuwa ni: kuondoa nongo (uchafu) wote, mabaki ya majasho na kuiagua ngozi iliyofifia, pili kuliondosha vuzi la mwili (vinywele vyembamba mwilini) na kuufanya mwili uwe mororo.

Kwa madhumuni ya kwanza na ya pili walitumia sandali. Na kusudio la tatu wakisingwa kwa mafuta El- maawy (2011). Tunaunga mkono maoni ya wataalamu hao na kueleza kuwa kusinga ni kitendo cha kumsuguwa mtu aidha kwa dalia na marashi, kwa sandali au liwa, kwa karafuu na mafuta, kwa ajili ya kuondoa nongo alizonazo mwilini mwake na kuufanya mwili uwe safi na laini. Bi. Harusi hufanyiwa singo kwa ajili ya kutoa nongo mwilini mwake na kuwa mororo, ili anapoolewa na kwenda kwa mume wake mwili uweko laini na mororo.

Somo yake Kukuwa alimtayarisha mwari wake kwa kuanzia na singo. Somo huyu alitafuta watu watatu kwa ajili ya kumsinga Kukuwa (585 na 586). Mila na desturi za wanawake hawa ni kusingana juu ya mkeka na mtu anaesingwa hupakatwa mapajani (587). Mwandishi anatueleza kuwa Kukuwa alisingwa juu ya mkeka ambapo alipakatwa mapajani. Wasingaji hao walimsinga Kukuwa kwa kutumia dalia na marashi, (583 na 584). Baada ya kumaliza kumsinga walimpeleka chooni na kumuogesha baadae walimvalisha kanga mpya.

Baada ya singo somo alimtafutia mwari wake mpakaji wa hina, hivyo Kukuwa alipakwa wanja miguuni na mikononi na wanja ndio uliokuwa ukichorewa maua hayo (579 – 582). Siku yakuo inapofika wazazi wa mume hupeleka mjumbe kwao Bi. Harusi kuhusiana na kuo na kuingia ndani. Mjumbe anaepokeleka habari huingia kwa siri na taarifa alizotumwa huzitoa kwa siri. Siku hiyo huwa inatazamwa kwa watabiri na wazazi husoma dua mbalimbali ili siku hiyo ipite salama. Haya tunayapata katika katika beti za (589 – 592) katika beti za (591 na 592) msanii anasema,

591. *Hiyo huwa siri sana*
Husemwa kwa kunong'ona
Huletwa usiku sana
Kwa saa itomkini.

592. *Siku hiyo hutazamwa*
Au tuseme hupimwa
Kwa madua yakasomwa
Hamna cha upinzani.

Mila na desturi za wanawake wa visiwani hapo kale, siku ya harusi ianpofika Somo humuogesha mwari wake na baadae humfukiza manukato mbalimbali kama vile udi ili anukie. Mwandishi ameyazungumza haya katika beti za (600 na 601). Baada ya Kukuwa kuogeshwa na kufukizwa udi Somo yake alimsuka nywele nzuri, alimvalisha kanga za kisutu na utunda (ushanga) tumboni na kiunoni na baadae alimuweka kitandani na kumsubiri muumewe.

Pia wanawake wa zamani waliwafunga watoto wao wanaoolewa kisarawanda (kitambaa cheupe) kiunoni kwa lengo la kuangalia kizinda (610). Hapo mwari hufundishwa ya kuwa asifanye vita wakati mume anapoingia ndani, hii ni kwa sababu wazazi wake na wazazi wa muumewe wanasubiri kizinda chake (611 - 615). Katika beti za (611 na 612) msanii anasema,

611. *Maneno aloelezwa*
Kungwile kamueleza
Matata kutofanza
Bwana akingiya ndani.

612. *Kwamba wazazi wake*
Waume na wanawake
Wangoja kizinda chake
Asifanye ubishani.

Kwa mila na desturi za visiwani bwana harusi anapokuja kungia ndani, huja na watu watatu si zogo la watu na huja kwa siri. Somo ndie anaempokea na kumkaribisha katika chumba alichoko mkewe. Katika utenzi huu tunamuona

Somo yake Kukuwa akimkaribisha bwana harusi katika chumba cha mkewe. Baada ya kuingia ndani mume hutakiwa atoe ada, na baadae somo humtaka avue nguo zake na hupewa kanga iliyofukizwa manukato na bwana huvaa kiunoni. Msanii ameyazungumza haya katika beti za (618 – 625). Baadae somo alimkaribisha muumewe Kukuwa chakula na kumuonesha kisarawanda alichofungwa Kukuwa (622 - 625). Somo huyu alimfundisha bwana harusi jinsi ya kufanya jimai (tendo la ndoa), ili aweze kuidhihirisha bikra ya mkewe (629 na 630). Baada ya hapo somo alitoka chumbani na kuufunga mlango kwa nje, kwa siku hiyo alilala chini ya kizingiti ili kusubiri majibu ya walio ndani.

Ni wajibu wa Bwana Harusi kuugonga mlango wa chumba alichokuwemo baada kumaliza shughuli yake. Hapo somo hufunguwa mlango kwa wasiwasi kwa sababu hajui kilichotokea ndani. Msanii anatueleza haya katika beti za (633 na 634). Katika beti hizo msanii anasema,

633. Bwana akiwa tayari

Huwa nayo kubwa ari

Bila ya kutahayari

Ngo, ngo, kutoka ndani.

634. Somo hapo hugutuka

Kiuno akakishika

Rohoye kutikisika

Hayajuwi kuna nini.

Bwana harusi alipogonga mlango, somo aliingia ndani na baada ya kuona mambo ni mazuri, aliwaita jamaa wote wa mtoto wa kike na mtoto wa kiume ili waje wajionee kizinda cha mtoto wao, (637 – 640). Baada ya hapo somo alimuondosha Kukuwa na kuanza kushangiria kwa vigelegele na kuimba

nyimbo za kupeana hongera, vilevile walipakana masinzi kama ishara ya kuwajulisha watu wengine kwamba mtoto wao ameonekana kizinda (bikra) (641 – 644).

Kwa mila na desturi za wanawake wa visiwani hapo zamani ikiwa mtoto wao aliyeolewa ataonekana kizinda, hutunzwa tunza mbalimbali kwa ajili ya kumpongeza kutokana na heshima na uaminifu aliouonesha. Mume na wazee wake pamoja na wazazi wa mwanamke ndio wanaomtunza Bi. Harusi, zawadi hizo zinaweza kuwa: bangili za dhahabu, kidani cha dhahabu na vitu vyenginevyo, (649 na 650). Katika beti hizo mwandishi anatueleza kuwa Kukuwa alitunzwa bangili na kidani cha dhahabu kutoka katika familia ya mumewe. Pia wazazi wake Kukuwa walimtunza mtoto wao kipini na kikuku kutokana na jitihada yake ya kujiheshimu na kujilinda na baadae kuwafurahisha wazazi wake kwa kuonekana kizinda, (625). Baada ya kumaliza shangire zao za kupeana pongezi somo hakumuacha Kukuwa na uchafu wake bali alimbeba na kumpeleka chooni na kumuogesha janaba. Katika beti ya (668) msanii anasema,

668. Kwanza hutawazishwa

Halafu tena hukoshwa

Janaba kuiondosha

Limuondoke mwilini.

Kukuwa alipomaliza kuogeshwa alirudishwa chumbani na kuwekwa kwenye kiti cha henzerani, na kuwekwa chetezo chenye udi ili udi uingie ndani. Udi huu kwa mila na desturi za wanawake hawa, ulikuwa ni dawa kwa

mwanamke mwari aliyefanya jimai (tendo la ndoa) kwa mara ya kwanza. Dawa hii ilifanywa ili asije akaumia siku za mbele anaporudia tendo la ndoa. Zoezi hili hufanywa kwa muda wa siku saba. Bi. Zaynab ameyathibitisha haya katika beti za (679 – 684).

Mwandishi anatueleza kuwa siku inayofuwata ilikuwa ni siku ya kuingia nyumbani (686). Siku hiyo hualikwa watu na kuwekwa ngoma mbalimbali kama vile lelemama, tarabu n.k. Siku hiyo Bwana Harusi hutoka kwao na wapambe wake wawili, kipando alichokuwa akipandishwa kilikuwa ni gari au farasi. Baada ya Bwana Harusi kuwasili, hufunguliwa mlango wa gari na kutoka baadae hupelekwa mjumbe kwa wazazi wa mwanamke kuwajulisha uwepo wa mkwe na wao (wazazi wa Bi. Harusi) huwenda kuwapokea. Kama tulivyoielezwa na mwandishi katika beti za (687 – 689, 695 – 698, 702, 712, na 714).

Kwa mila na desturi za hapo zamani, Bwana Harusi alikuwa hafunguliwi mlango wa chumba alichu mkewe baada ya kuwasili, mpaka atoe pesa ambazo huitwa kifunguwa malango, pindi tu pesa zinapotolewa mlango hufunguliwa na Bwana Harusi huwa huru kuingia ndani, bwana harusi anapoingia ndani huwa haingii na kundi la watu, bali huingia peke yake. Na hapo huwachwa ndani yeye na mkewe. Katika beti za (720 – 724) mwandishi anayathibitisha hayo.

4.4.3.2.4 Kipindi cha Baada ya Ndoa

Kwa kawaida wanawake wa zamani walizifanya harusi zao kwa muda wa siku saba, ambazo waliziita siku za fungate. Siku hizi zilianza siku ya pili

baada ya Bwana Harusi kuoa. Siku hzi saba walikuwa wakipika vyakula aina mbalimbali, vyakula hivi alipikiwa Bi. Harusi pamoja na wageni mbalimbali waliohudhuria. Wazee wa Bi. Harusi walivipika vyakula hivi mpaka siku mtoto wao atakapotoka ndani na kwenda nyumbani kwake. Katika beti za (735 – 742, 807 – 811) mwandishi anatueleza hayo.

Baada ya harusi kwa mila na desturi za wanawake wa zamani, siku ya tatu ilikuwa ni siku ya kuonesha kizinda. Bi. Harusi alivalishwa nguo nzuri na kupambwa kwa mapambo mbalimbali na kutolewa nje, ambako huwa kuna ngoma ya lelemama. Baada ya hapo somo huenda ndani na kumpa mkubwa wa chama chao upatu ambao ndani yake umetiwa kizinda cha Bi. Harusi. Kizinda hicho hutolewa hadharani na kuonesha watu waliohudhuria. Mila na desturi hii ilifanywa kwa lengo la kuwafunza wari ili wawe na moyo wa subira na kujitunza, ili na wao waonekane bikira pindi watakapoolewa. Katika beti za (774, 783, 784 – 788) mwandishi anatusimulia jambo hilo pale ambapo kizinda cha Kukuwa kilipotolewa nje na kuonesha watu wote waliohudhuria ghafla hiyo.

Baada ya somo kukionesha kisarawanda chenye kizinda, alizionesha na tunza alizotunzwa Kukuwa na familia ya muumewe pamoja na wazazi wake. Katika beti za (790 – 792), msanii anatueleza kuwa baada ya somo kuonesha kisarawanda alivionesha vitu ambavyo vililetwa na mume wake Kukuwa. Mambo haya yalifanywa na wanawake watupu na waliyafanya ndani. Ilikuwa hathubutu mwanamme yeyote kuingia humo. Katika ubeti wa (795) msanii anasema,

795. *Mwanamme hathubutu*

Kuingia kwenye watu

Wapigaji ni wao tu

Huwapo hapo bandani.

Kwa kawaida harusi za visiwani hapo kale na baadhi yao hivi sasa, wazazi wa watoto wanaoozesha walipika lima (karamu) kwa ajili ya kuwalisha watu waliowaalika harusi. Katika utenzi wa *Mwana Kukuwa*, mwandishi anatueleza kuwa siku iliyofuwata baada ya kuoneshwa kizinda, ilikuwa ni siku ya lima (karamu). Karamu hii ilifanywa kuukeni (804). Siku hiyo hupikwa biriani na kulishwa watu waliohudhuria, kama walivyofanya wazazi wake Kukuwa, (805 na 806).

Mwandishi anaendelea kutueleza kuwa, siku sita za fungate zilipokwisha, wazazi wa mwanamme walifanya maulid ya Mtume (S.A.W). Maulid hayo yalisomwa na wanaume, (815 – 819). Inapofika siku ya saba Bi. Harusi alitoka kwenye fungate (871). Siku zote saba Bi. Harusi alisuguliwa ili kuondoa uchafu alionao (872).

Baada ya lima (karamu), siku ya kumtoa Bi. Harusi kwenye viatu iliwadia. Somo aliwaalika watu kwa ajili ya kuja kumtoa mwari wake kwenye viatu (876). Katika sherehe hiyo palihitajika mchele vibaba vitatu, shilingi tatu, na kidani cha fedha. Vitu hivyo vilitiwa kwenye upatu pamoja na mchanga wa baharini na kuwekwa katika kizingiti cha chumba alichu Bi. Harusi (892 – 894). Upatu huo uliwekwa kizingitini ili Bi. Harusi auruke mara tatu wakati atakapotoka ndani (896 na 899). Katika beti hizo msanii anasema,

896. *Cha chumbani kizingiti*

Mchanga huwako kati

Auvuke bibi ati

Akitoka huko ndani.

899. *Huuruka mara tatu*

Huku kavaa viatu

Vitawanda si sapatu

Alovaa miguuni.

Baada ya Kukuwa kuuchupa upatu huo, alipelekwa ukumbini kwa ajili ya kupewa wasia na mafunzo mbalimbali. Miongoni mwa mafunzo aliyyopewa ni: kumpokea mumewe, kumpa maneno ya kuliwaza, na hayo alitakiwa ayafanye hadharani kwanza. Haya yote tunayapata katika beti za (912 - 914).

Bi. Zaynab anatwambia kwamba zinapomaliza shughuli hizo zote hubakia siku ya Bi. Harusi kupelekwa kwake. Kwa mila na desturi za wananwake hawa waliitazama siku hiyo kwa ajili ya kuitafuta siku sahihi (935 – 937). Kwa kawaida siku hiyo hutolewa na waume (951) lakini na wanawake ni lazima waseme kama siku hiyo inafaa kwa mujibu wa maelezo ya mwalimu aliyewatizamia. Baada ya kuwafikiana hutumwa mjumbe ili aipeleke siku na saa na kwa kawaida yao ilikuwa ni usiku wa saa mbili (956 na 957), hapo huitwa somo ili kujulishwa siku hiyo (960 na 963).

Mila na desturi za wanawake hawa kabla ya mtoto wao kumpeleka kwake, waliwatafuta mashekhe au walimu wanaojua kusoma dua za kumfunga mtoto, kueuliwa na kuzinguwa (967 na 968). Mtoto alizunguliwa kama dawa ya kumuepusha na husda mbalimbali. Mwandishi ameyazungumza haya katika ubeti wa (971). Siku ya kupelekwa kwake, Kukuwa alisuguliwa kwa dalia na tibu, alipakwa hina, na wanja ili appendeze na kung'ara zaidi, wakati

atakapokwenda kwa muumewe, (974 – 976, 979 – 981). Kabla Kukuwa hajapelekwa kwake kwanza alipelekwa mtoto wa miaka kumi aliyevalishwa vizuri na kupewa mswala na Msaafu avipeleke nyumbani kwa Kukuwa. Lengo na madhumuni ya vitu hivyo ni kuwa, bwana na bibi harusi wafanye ibada ya kuswali na kusoma Qur-ani kabla ya kulala. Msanii ameyazungumza hayo katika beti za (997 – 1002).

Wakati wa kumpeleka Bi. Harusi ni mila na desturi hapo zamani kutafuta mayai matatu na mtu wa kwenda kuyavunja mayai hayo mlangoni kwa Bi. Harusi. Baada ya kwisha vunjwa huyakiuka (huyachupa) ndipo huwa huru kuingia ndani. Katika beti za (1028 – 1030) msanii anatuelza mambo hayo. Wakati wa kuyavunja mayai hayo huwa kuna masharti, mtu aliyepewa kazi hiyo huwa hayavunji tu, mpaka apewe amri. Wakati wa kuyavunja hutakiwa amkamate Bi. Harusi mabega yake (1031 – 1033). Bi. Zaynab anatueleza kuwa mila na desturi hii ilifanywa kwa lengo la kuondoa husda na madhara kwa Bi. Harusi. Katika beti za (1028 na 1030) msanii anasema,

1028. Hapewa hapo shihata

Mayai kuyakamata

Matatu akafumbata

Kiganjani vidoleni.

1030. Mlangoni hapo kwake

Bi. Harusi akiuke

Hunenwa au aruke

Kukanyaga mlangoni.

Bi. Harusi baada ya kupambwa vizuri, huvishwa baibui la kizoro na kitambaa hushushwa ili asionekane. Huingizwa kwenye gari na kupelekwa kwake. Somo wa Bi. Harusi hutangulia mbele kwa lengo la kumpa saini mtu wa kuvunja

mayai. Bi. Harusi anapofika kwake huyakiuka na kuingia ndani kwenye chumba chake. Baadae, wazazi wake pamoja na somo humfunza tena mambo mbalimbali ya jinsi ya kukaa vyema na mume wake pamoja na wakwe zake. Mwandishi ametudhihirishia hayo katika beti za (1034, 1036, 1046, 1048 – 1050, 1054 na 1058).

Bi. Harusi anapofika kwake haachwi tu peke yake na watu wakaondoka, mwandishi anatwambia kuwa, Kukuwa alipofika kwake alikabidhiwa kwa wakweze na wakwe zake nao walimpokea (1068 – 1074). Baadae aliitwa muumewe chumbani ili na yeye akabidhiwe mkewe na ayasikie mambo yatakayozungumzwa (1075 – 1083). Mara tu Kukuwa alipokabidhiwa kwa wakwe na muumewe, baadhi ya watu waliondoka na walibakia mama yake mzazi, bibi na somo kwa ajili ya kumfunza na kumuusiya mtoto wao. Somo alibakia kwa muda wa wiki mbili kwa ajili ya kumfunza na kumwangalia je, mambo aliyomfunza anayatekeleza (1085 - -1087, 1105 – 1107).

Baada ya hapo Bi. Harusi huusiwa mambo mbalimbali ya kuishi na wakwe zake na muume wake vizuri (1106 1107). Baadhi ya mambo aliyousiwa Kukuwa na somo yake ni: kuishi na mume vizuri, kuachana na mashoga, kutotoa siri za ndani, kupokea apewacho na kushukuru kwa asichopewa, kumtii mume wake kwa anayoyataka lakini yawe ni sheria ya dini, aishi nae kwa huruma, amfurahishe kwa kumfanyia mambo mbalimbali mazuri, amtilie mume wake manukato na mapambo wakati wa usiku, kuendeleza kazi alizofunzwa ili kumsaidia mume wake anapokuwa na shida, ampokee wakati anaporudi mahali popote palipowatenganisha, anapokuwa na hasira azifiche

asimuoneshe muumewe akajuwa, akishakula amuache apunzike, amkande mume wake, awaenzi wakwe zake n.k. Mwandishi anatuthibitishia haya katika beti za (1107 – 1136). Baadae mume nae alipewa mafunzo yake ya jinsi ya kuishi vizuri na mke wake (1138 – 1151).

Baada ya wasia wa somo, ulifuwata wasia wa mamaake mzazi (1154). Mama huyu alimuusiya mwanawe juu ya kumtunza mume wake, akiitwa asilegee, asimkere, awe mcheshi na asiwe mshawishi wa kuendeleza mzozo, asiwe mbadirifu, amfanyie mume wake analolitaka na aache kufanya asilolitaka mume wake, awaheshimu wakwe zake, afanye kazi alizofunzwa ili aweze kukidhi mahitaji yake, ashike Dini kwa kufuwata nguzo tano n.k.

Haya tunayapata katika beti za (1170 – 1169). Hapo Bi. Kukuwa alijibu kwa kutoa ahadi ya kuyatekeleza aliyousiwa kwa kumtunza mume wake (1174 na 1175). Mwisho kwa mila na desturi za wanawake hawa baada ya kumuusiya mtoto wao na mkwe wao mausio mbalimbali, huwaita wakwe chumbani walimo watoto wao na kuwakabidhi mkwe wao tena, kwa mara ya mwisho, kwa kupewa nasaha mbalimbali. Miongoni mwa nasaha walizopewa wakwe zake Kukuwa ni: kukaa vyema na mkwe wao, akikosea wamwambie wasimfanyie nongwa, wakae nae kwa wema ili wasije wakaharibikiwa, kwani siku zote binaadamu hawapendi kuwaona watu wakiishi vizuri. Nasaha hizi tunazipata katika beti za (1179 – 1188).

4.4.3.3 Ngoma za Asili

Neno “ngoma” lina maana mbili: ngoma ni ala ya muziki inayotengenezwa kwa kuambwa ngozi kwenye mzinga, lakini linaloitwa “ngoma” vilevile ni

maonesho ambayo yanataka kuwepo kwa mziki, mchezo na wimbo. Hivyo, vitendo hivi vyote vitatu kwa wakati mmoja vinafanya maonesho yaitwe ngoma. Maonyesho ambayo ndiyo utamaduni wa Mswahili. Kwa kawaida wasanii wanaopiga ngoma huwa ni wanaume, isipokuwa katika ngoma za unyago, wakati ambapo watoto wa kike wanapopata ukubwa, wanakaribishwa katika jamii ya wanawake. Wanaume na wanawake wanaweza kucheza na kuimba pamoja, isipokuwa kuna baadhi ya ngoma za kiasili ambazo ziko zinazowahusu wanawake peke yao na ziko zinazowahusu wanaume peke yao. Brunotti (2005).

Kwa mujibu wa Ismail (2011) anasema ngoma ni uchezaji wa viungo vya mwili kwa mnyambuliko na utaratibu maalum katika mapigo ya ngoma yenyewe, ala, kulingana na kabila husika na desturi zake.

Katika mila na desturi za Waswahili, ngoma ni kitu muhimu sana katika maisha yao ya kila siku. Hii ni kwa sababu ni mila ambayo inawafunza watu tangu utotoni mwao. Vilevile ngoma ni aina ya sanaa, kwa hivyo inazaliwa, inaishi na inakufa. Wakati ambapo ngoma inapoonyeshwa inahusu wasanii pamoja na watazamaji. Kutokana na tabia hizo mbili, ngoma inakuwa pahala pa kuisoma jamii, historia, siasa, na dini. Kwa kawaida ngoma hazichezwi ili kuwafurahisha watu kama kiburudisho tu, zaidi huchezwa kwa sababu ni mojawapo ya sehemu ya maisha ya Waswahili. Ngoma huishi kwa ajili ya kuendeleza utamaduni ambao umezaliwa kwenye jamii. Hata hivyo inailisha jamii hiyo na kuilinda hasa.

Hapo zamani mababu zetu walitumia ngoma kama chombo cha mawasiliano, katika makabila mengine ngoma ilitumika kwenye sherehe mbalimbali kama chombo kikuu cha kutolea burudani. Ngoma zilitumika kwenye jando na unyago na hata baada ya kazi kama chombo cha kutolea mafunzo, maonyo au kuiasa jamii ijikosowe kwa njia ya nyimbo zinazotungwa. Nyimbo za ngoma zilitumika kama ishara ya jambo fulani, hali hii ilipelekea kufikisha taarifa katika vijiji vingi sana, hii ni kwa sababu ngoma ilisikika sana.

Katika visiwa vya Zanzibar ngoma huchezwa katika sherehe mbalimbali kama vile sherehe za kisiasa, za dini na jadi kama vile skukuu ya mwaka kogwa inayosherehekewa Makunduchi (Kusini Unguja) na sherehe ya kuoga mwaka inayofanyika Kojani (Kaskazini Pemba). Pia ngoma huchezwa katika sherehe mbalimbali ambazo huitwa wasanii ili waoneshe ngoma za utamaduni wa Kizanzibari. Halikadhalika ngoma zinapingwa na kucheza kwenye Mahoteli ya kitalii ili watalii wapate kuona utamaduni wa Kizanzibari japo kidogo.

Tukiangalia mila na desturi hii ya ngoma za asili kwa upande wa visiwani tunaona kuwa, hapo zamani Wazanzibari walikuwa na aina mbalimbali za ngoma, ambazo ziliimbwa na kucheza katika sherehe mbalimbali. Ngoma hizo baadhi yake zinapatikana hadi sasa, na baadhi yake zimeshakufa, hii ni kwa sababu wapigaji na wachezaji wake baadhi yao wameshakufa na wengine ni wazee sana. Au tunaweza kusema kuwa baadhi ya ngoma hizo zimekufa kutokana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yaliyoikumba jamii ya Kizanzibari na jamii nyengine kwa ujumla.

Katika utenzi wa *Mwana Kukuwa*, msanii anatueleza kuwa wanawake wa visiwani hapo zamani, walikuwa na vyama vya ngoma ambavyo vilipiga na kucheza ngoma za aina mbalimbali kama vile: msewe, lelemama, beni, msondo, maulidi, tarabu, boso, msewe, bomu na nyingi nyenginezo. Ngoma hizo zilipigwa katika sherehe mbalimbali kama vile: sherehe za harusi, sherehe za kuwakaribisha viongozi, sherehe za unyago n.k. Kwa mfano katika beti za (687 – 690) msanii anatueleza kuwa, katika harusi ya Kukuwa kulialikwa vyama vya ngoma kama vile: lelemama, beni, bomu (473) na vyenginezo kwa ajili ya kwenda kutumbuiza. Katika beti za (687 – 690) msanii anasema,

687. *Hualikwa wingi watu*

Wanawake kutukutu

Si wengi wakafurutu

Lelemama uwanjani.

688. *Pengine huwa tarabu*

Vyama nao wakitibu

Pia nao watiribu

Waliokuwa zamani.

689. *Vilikuwa vingi vyama*

Vya kucheza lelemama

Ilikuwa kubwa ngoma

Ikivuma ungujani.

690. *Na mume upande wake*

Ilikuwa ngoma yake

Pia itokee kwake

Ngoma hiyo ni ya beni.

Iwapo katika jamii ya Kizanzibari hapo zamani pakitokea sherehe ya harusi au sherehe nyengine yoyote ile iwayo, vyama hivyo vilikodiwa kwa ajili ya kutumbuiza katika sherehe hiyo. Katika beti za (475 – 477) msanii anatuthibitishia hayo. Katika beti za (478 – 481), mwandishi anawambia kuwa Bibi yake Kukuwa alikialika chama cha lelemama kwa ajili ya kufanya jaliko

na kutumbuiza katika harusi ya mjukuu wake. Katika beti za (478 na 480) msanii anasema,

478. Mambo yalipoumana

Bibi akasema tena

Kamwiteni shekhe tena

Tumtake samahani.

480. Kwamba twataka jaliko

Na shinda pia iweko

Lelemama takuweko

Nalo bomu uwanjani.

Kutokana na Nadharia ya Sosholojia tunaweza kusema kuwa, wanawake wa zamani, walikuwa wakipiga na kucheza ngoma mbalimbali ambazo zilikuwa ni sehemu ya mila na desturi zao kwa ajili ya kuuenzi na kuulinda utamaduni wao wa Kizanzibari. Ngoma hizo zilipigwa na kucheza kama ni kiburudisho na ni chombo cha kutolea maonyo kwa jamii hiyo, katika Nyanja mbalimbali za maisha kama vile kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

4.4.3.4 Tiba za Asili

Kwa mujibu wa BAKIZA, (2010) tiba ni dawa au maelezo anayopewa mgonjwa ili kuponya maradhi yake. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa, tiba za sili ni ujuzi wote wa njia zinazoelezeka na zisizoelezeka za uchunguzi, zinazohusisha mimea ya asili kutengeneza madawa ya asili ya uzuwiyaji na uondowaji wa hali isiyo ya kawaida katika afya ya binaadamu na mimea.

Tunaposema tiba za asili tunamaanisha tiba inayotumia dawa za asili zinazotokana na majani, magome ya miti, mizizi, na matunda kwa ajili ya kunywa, kupaka, kuchua na hata kunusa. Tiba ya asili imeitwa hivyo kwa

sababu inatokana na mimea ya asili. Pia ni kitu kilicho wazi na cha asili kinachopatikana katika maeneo tunayoishi.

Tiba ya kutumia madawa asilia ilikuwepo kabla ya ujio wa Wakoloni, ambapo mababu zetu waliitumia kwa ajili ya kutibu maradhi yaliyoibuka katika jamii zao wakati huo. Wakoloni walipoingia nchini ndipo walipoleta dawa za vidonge, dawa za maji (vimiminika) na matumizi ya sindano. Matumizi ya dawa za asili au tiba mbadala yameenea kwa sasa. Hii ni kutokana na kwamba dawa za asili zimejipatia umaarufu katika sehemu mbalimbali duniani kutokana na kupigiwa debe muda mwingi.

Wanawake wa visiwani hapo zamani na hadi sasa, walitumia dawa mbalimbali za asili kwa ajili ya kujilinda na kuondosha maradhi yaliyowathakili. Dawa hizo aidha zilikuwa za majani, mizizi, magome ya miti, au tunda za miti ambazo zilitumika kwa kunywa kujipaka au kuchua. Miongoni mwa dawa zilizotumika ni: mvuje, habasoda, mafuta ya nazi na mafuta ya halizeti yaliyochanganywa na madawa mengine, majani ya mbono (mbarika), mizizi ya mtopetope, mkuwa usiku, asali, ndimu, uwatu, muinga jini, mvuje na nyingi nyenginezo, ambazo zilitumika katika kutibu maradhi mbalimbali.

Katika utenzi wa *Howani* msanii anatueleza kwamba, wanawake wa zamani katika visiwa vya Unguja na Pemba, walizilea mimba zoa na watoto wao kwa madawa ya asili ambayo walipewa na Bibi Mkunga au mtu mwenye ujuzi wa dawa hizo katika mitaa au vijiji vyao. Katika beti za (13 na 45) msanii anatueleza kuwa, mara mwanamke anapobeba ujauzito alipewa madawa

mbalimbali kama vile mvuje na habasoda kwa ajili ya kuondosha maumivu na kumkinga mjamzito na vijicho na mashetani wabaya.

Vilevile katika beti za (78 – 80) msanii anatueleza kuwa baada ya mjamzito kujifunguwa, hufukizwa kwa madawa mbalimbali katika chumba chake. Pia hukandwa kwa kutumia majani ya mbarika (mbono) kwa ajili ya kuufanya mwili wake uwe laini. Wanawake hawa waliwasinga wazazi wao kwa kutumia mafuta ya zeti (zaituni) kwa sababu yaliufanya mwili wa mzazi uwe madhubuti, na uweze kujirudi kwa haraka.

Ama kwa upande wa mtoto mchanga aliyezaliwa, alifukizwa kwa madawa mbalimbali pamoja na kufungwa mvuje uliochanganywa na chumvi mikononi mwake. Katika beti za (68 na 141) msanii anasema kuwa Kukuwa alifungwa mvuje mkononi mwake na kufukizwa kwa mvuje ili kumuepusha na madhara yaletwayo na majini. Katika beti hizo msanii anasema,

68. Mvuje wako kafungwa

Mkono ukaviringwa

Na nyeusi yako kanga

Ukafunikwa kwa shani.

141. Hufungwa ile mivuje

Na mafusho tejeteje

Kwa hayo ili afuje

Yaletwapo na majini.

Hivyo, kutokana na Nadharia ya Sosholojia, tiba za asili za kutumia miti shamba ni mila na desturi zilizomo katika jamii za watu katika makabila mbalimbali. Tiba hizi huweza kufanana au kutofautiyana kutokana na jiografia ya maeneo mbalimbali wanayoishi binaadamu.

4.4.3.5 Mapambo/Urembo wa Wanawake wa Visiwani

Kwa mujibu wa (Paneli la Kiswahili) wanasema kuwa mapambo ni vitu vinavyovaliwa na watu ili kujirembesha, kuwafanya wavutie machoni pa watu wengine. Mapambo yanaweza kuwa bangili, herini, hina, utunda (shanga), vikuku, kipini, mafuta, mkufu, mkanda, pete, poda, rangi ya mdomo, wanja n.k. Urembo ni mapambo anayojitia mtu ili apendeze, hali ya kuwa mmaridadi. BAKIZA (2010). Tunaunga mkono maoni ya wataalamu hapo juu na kusema kuwa, mapambo au urembo ni vitu vinavyotumiwa na wasichana na wanawake kwa ajili ya kujirembesha na kuonekana warembo machoni mwa watu. Vitu hivyo vinaweza kuwa vya kuvaa kama vile herini, bangili, kidani, pete shanga n.k. Na vitu hivi vinaweza kuwa vya dhahabu, fedha au kareti. Vilevile vinaweza kuwa manukato na maua yenye kunukia kama vile: hal-udi, udi, mafuta mazuri, manargisi, mawardi, asumini, afu n.k.

Urembo na utanashati ni sifa za tangu asili za wanawake wa visiwani. Wanawake hawa walijipenda, walijijali, walijitunza na walikuwa ni wamaridadi. Vilevile hawakutegemea urembo wa kughushi. Hina, wanja, udi, mawardi, asumini, vilua, mipachori, mirehani, minargisi, vikuba, liwa, sandali, karafuu, dalia na mengineyo, ni baadhi ya msamiati unaoambatana na urembo na kujiremba kwao. Wanawake wa visiwani walijiremba wakati walipokwenda kwenye shughuli mbalimbali, wanapokuwa na waume zao nakadhalika.

Kutokana na Nadharia ya Sosholojia mwandishi Bi. Zaynab Himid katika utenzi wake wa *Mwana Kukuwa*, anatwambia kuwa wanawake wa visiwani walijipamba na kujirembesha kwa kutumia mapambo na manukato mbalimbali

wakati walipokuwa na shughuli maalum kama vile: kwenye harusi, kwenye ngoma na sherehe nyenginezo. Katika utenzi huu mwandishi amewachora wahusika wake wakiwa wamejipamba na kujiremba kwa mapambo mbalimbali katika kipindi cha harusi ya Kukuwa. Kwa mfano, mwandishi anatuonesha jinsi Kukuwa alivyosukwa nywele nzuri (usuluti) na katikati ya nywele hizo alifungwa kikuba ambacho kilitumika kama ni pambo la nywele (749). Vilevile katika beti za (750 – 754, 891) mwandishi anatueleza kuwa, Kukuwa alipambwa kwa mapambo mbalimbali kama vile dhahabu, bangili, vikuku na mkufu, pia alitiwa vigurudumu na vitana vya dhahabu katika nywele zake.

Somo yake hakuacha kumpamba mwari wake kwa kutumia herini, kipini cha pua pamoja na pete ambazo zilimfanya apendeze kupita kiasi. Kukuwa hakuachwa kutiwa asumini na kuvishwa vikuba katika shingo yake ili apendeze na aonekane nzuri. Mwandishi ameyaeleza haya katika beti za (751 na 891) msanii anasema,

751. Bangili pia vikuku

Havishwa huku na huku

Na mikufu pakupaku

Akavalishwa shingoni.

891. Asumini na vikuba

Vyenye wingi wa haiba

Shingo yake ilibeba

Na kuenezwa kichwani.

Mwandishi anaendelea kusema kuwa Kukuwa alipotaka kuolewa Somo yake alimpaka hina na wanja (516). Vilevile wanawake wa visiwani watoto wao walioolewa wakati wanapoonekana bikira huwatunza mapambo mbalimbali kama vile: mkufu, bangili, hirini n.k Katika beti za (649, 650 na 653)

mwandishi anatueleza kuwa baada ya Kukuwa kuonekana kizinda alizawadiwa bangili na kidani cha dhahabu kutoka kwa wazazi wa muumewe. Wanawake hawa walifanya hivyo kwa lengo la kuthamini mapambo au urembo ambao ni miongoni mwa mila na desturi zao kufanya hivyo.

4.4.3.5 Mavazi ya Wanawake wa Visiwani

Mavazi yanaweza kuwa nguo, viatu, mkanda, miwani, ambayo kwa kawaida huvaliwa kwa lengo moja tu la msingi ambalo ni kumsitiri mtu na kuficha aibu ya utupu wa mwanadamu. [Http://www.ackyshine.com](http://www.ackyshine.com). Kipindi hiki cha sayansi na teknonolojia, mavazi huvaliwa kwa ajili ya sababu mbalimbali, zikiwemo na kujilinda dhidi ya athari za hali ya hewa, mazingira, kazi na uchafu.

Wengine huvaa nguo ili kuonesha heshima katika jamii au kutowakwaza wengine. Wapo baadhi ya watu wanaovaa mavazi kwa lengo la kujipamba na kupendeza. Lakini kwa wengine mavazi huwa ni kitambulisho cha utaifa na kazi, kama vile: nguo za michezo, sare za shule, nguo za askari, sare za wafungwa n.k. Ingawa nguo zimewekwa kumtambulisha mtu na kazi yake au tabia yake, watu wengine huvaa nguo ili kuficha utambulisho wao. Baadhi ya watu huvaa nguo kwa lengo la kuonesha uwezo wao wa kiuchumi katika jamii.

Wanawake wa visiwani hapo zamani walivaa mavazi ambayo yaliendana na mila na desturi zao za Kizanzibari. Baadhi ya mavazi ambayo walivaa ni: shimizi, kanchiri (sidiria), kilemba, ubinda, hafu, kaniki, ukaya (kitambaa cha

usoni), buibui/baibui, mitandio, suruali za marinda n.k. Baadhi ya mavazi hayo yalivaliwa katika sehemu mbalimbali kama vile: harusini, katika sherehe za ngoma nakadhalika.

Tukirejelea katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*, tunaona kuwa wanawake hawa walivaa mavazi mbalimbali kulingana na shughuli walizozifanya au safari walizokwenda. Katika beti za (52 na 78) mwandishi anatueleza kuwa wapelelzi waliokwenda kupelelza kwao Kukuwa walivaa mavazi ya asili ambayo yanaendana na mila na desturi zao. Walivaa buibui na kanga mbili na ushungi ambayo yalikuwa ni mavazi asilia. Katika beti hizo msanii anasema,

52. *Kangia nikamjuwa*

Uso hakujifunuwa

Baibui hakuvua

Kajipweteka kitini.

78. *Kanga mbili kavalia*

Mavazi ya asilia

Ushungi kajitupia

Miguu kaponi chini.

Vilevile katika jaliko wanachama wa lelemama na Bibi yake Kukuwa walivaa mavazi ya mila na desturi zao ambayo yanaendana na jamii yao. Katika beti za (490 – 494) mwandishi anatueleza kuwa Bibi yake Kukuwa alivalia kanga za kisutu, alijifunga ukaya pamoja na kigwe. Vilevile mashekhe wa ngoma walivaa kanzu na suruali za marinda na vichwani mwao walivaa vilemba (494 na 495). Bi. Zaynab anaendelea kusema wacheza bomu walivalia mavazi ya utamaduni kama vile suruali za marinda na walijitanda na mtandio (518 - 519).

Wanawake hawa walipopeleka mahari kwao mwanamke waliyekwenda kumposa, walimtafuta mtoto wa kike ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi

na walimvalisha nguo nzuri kwa ajili ya kuyapeleka mahari. Katika utenzi wa *Mwana Kukuwa* mwandishi anatuonesha kuwa, wazazi wake muumewe Kukuwa walipopeleka mahari walikivisha kitoto cha miaka kumi kanzu ya marinda, kilemba na sapatu.

Mtoto wa kike alipotaka kuolewa wanawake hawa walimvisha mavazi yanayoendana na utamaduni wao. Kwa mfano Kukuwa alipoolewa alivalishwa kanga za kisutu ambazo zilitumiwa sana kwa ajili ya kuwavisha maharusi (603). Katika beti za (747 na 748) mwandishi anatwambia kuwa Kukuwa alipoolewa alivishwa kanzu nzuri na mtandio ambazo zilimpendeza vizuri sana. Katika beti za (747 na 748) msanii anasema,

747. Kanzu ya namna yake

Mekaa mahala pake

Mwache mwari asifike

Lipofika uwanjani.

748. Kukuwa alivalishwa

Kanzu yake mshawasha

Hamkaa ya kutosha

Na mtandio kichwani.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa, wanawake wa visiwani walivaa mavazi yao ambayo yaliendana na mila na desturi zilizomo katika jamii yao. Mavazi hayo waliyavaa kwa ajili ya kujipendzesha, sherehe, harusi n.k.

4.5 Mbinu za Kifani

Fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira, Mbatiah, (2001), Wamitila, (2003), Njogu, na Chimerah (1999). Wamitila (2003) anaeleza kuwa , fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi ya kifasihi. Fani hueleza mbinu na

mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Hivyo, katika utafiti huu vipengele vya fani vilivyofanyiwa uchunguzi ni vile vinavyohusiana na mandhari, wahusika, lugha, pamoja na methali na misemo. Mtafiti alikusanya data na kuzichambuwa na kugunduwa kwamba, utenzi wa *Howani* na *Mwana Kukuwa* umetumia vipengele vya fani vilivyoielezwa hapo juu.

4.5.1 Mandhari

Tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*, zimeyachora maisha ya jamii ya Wazanzibari wa Unguja na Pemba ya wakati huo. Mandhari haya ni mandhari halisi ya visiwa vya Unguja na Pemba, ambayo ni miongoni mwa makaazi ya Waswahili.

Mandhari yanayojitokeza katika tenzi hizi, ni mandhari yakinifu yaliyotumiwa ni Bi Zaynab katika kueleza mila na desturi zilizofanywa na wanawake walioishi visiwani humo hapo kale. Katikla utenzi wa *Mwana Kukuwa* mwandishi ametaja kijiji miongoni mwa vijiji vinavyopatikana katika mji wa Unguja, kijiji hicho ni MATEMWE. Katika ubeti wa (190) msanii anasema,

190. Mambo sharti yatazamwe

Tusiyavamie kamwe

Hata tufike Matemwe

Tutayajuwa kiini.

Vilevile msanii amemalizia kwa kutaja mji aliozaliwa unaopatikana Unguja. Pia ameyataja mandhari ya visiwani pale alipotaja mahali anapoishi kuwa ni

Unguja ambayo imeungana na Pemba inayopatikana katika Jamhuri ya Tanzania katika beti za (396 na 397) katika *Utenzi wa Howani*. Katika beti hizo msanii anasema,

396. *L-hakira jina langu*

Amenipa baba yangu

Hapo kuzaliwa kwangu

Malindi ya Mkocheni.

397. *Naishi hapo Unguja*

Na Pemba yake ni moja

Yoyote ataekuja

Jamhuri Tanzania.

Hivyo, maelezo hayo ambayo ameyaeleza Bi Zaynab Himid katika tenzi zake, yanatupatia kufahamu mandhari halisi yaliyotumika katika tenzi hizi mbili. Mandhari yenyewe ni mandhari yanayowazunguka wanajamii wa visiwani (Unguja na Pemba). Hii ni kwa sababu mila na desturi zilizoelezwa katika tenzi husika zinapatikana katika mandhari hayo yaliyotajwa hapo juu.

4.5.2 Wahusika Katika Tenzi za Howani na Mwana Kukuwa

Wamitila (2010) anasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binaadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika vilevile hutambulishwa kwa maelezo ya wahusika wenzao au msimulizi. Utenzi wa *Howani* na *Mwana Kukuwa*, umetumia wahusika mbalimbali. Miongoni mwa wahusika waliotumiwa katika tenzi hizi ni: Sihadaike / Kukuwa, Mamaake Kukuwa, Baba yake Kukuwa, Bibi Mkunga,

Somo yake Kukuwa, Mume aliyemuoa Kukuwa, Baba wa Mume, Bi. Mrashi, Mshenga, Mpelelezi n.k.

4.5.2.1 Kukuwa/ Sihadaike

Sihadaike ama Kukuwa ndie muhusika ambae matukio na matendo yote yaliyomo katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* yanamuhusu yeye. Huyu ndie muhusika mkuu katika tenzi hizi. Mara tu Sihadaike alipozaliwa alifanyiwa mambo mbalimbali yanayohusu mila na desturi ambazo zilifanywa na mama yake. Mila na desturi alizofanyiwa ni kama vile kulazwa kwenye ungo uliotandikwa kanga kama kigodoro na mchanga kama mto n.k. Mtoto huyu alipotimia siku arobaini ndipo wazazi wake walipompa jina la Sihadaike. Katika beti ya (107) msanii anasema

107. Namwita Sihadaike

Dunia hii siyake

Hapo ndipo mwanzo wake

Ghururi zisimkhini.

Kukuwa alipofikia umri wa miaka sita, alipelekwa Chuoni kwa lengo la kwenda kuisoma Qur-ani (157 na 158) na alipotimia miaka saba alikuwa tayari keshamaliza msaafu (184). Sihadaike alipokhitimu wazazi wake walitoa ujira kwa mwalimu wake (185 na 186), na hapo alibakia nyumbani na mama yake akamfundisha zaidi kuijuwa dini yake na kujuwa kupika (191 na 192). Katika beti za (191 na 192) msanii anasema,

191. *Sihadaike kaka*

Nyumbani bila hadaa

Na mie sikusangaa

Nikamfundisha dini.

192. *Hamfundisha kupika*

Jikoni nikamuweka

Kuipua kuteleka

Na kutia sahanini.

Sihadaike alipotimia miaka kumi na mbili alivunja ungo (135), na hapo mama yake alimpeleka kwa somo yake ili afunzwe tohara na mambo mbalimbali yanayohusu maisha ili asije akaambiwa ni msungu (136 na 137). Mara tu alipopata hedhi kwa mara ya tatu Sihadaike alipelekwa unyagoni na somo yake na akafunzwa mambo mbalimbali yanayohusu umaridadi na maisha ya ndoa, katika beti za (245 – 249), na kutokana na maelezo ya mama yake Kukuwa aliyajuwa mafunzo yote aliyofundiashwa unyagoni (153).

Baada ya kurudi unyagoni Sihadaike alifunzwa kazi mbalimbali za amali na mama yake, miongoni mwa kazi alizofunzwa ni: kusuka ukili, kushona makawa, mikeka na misala, kutia nakshi mbalimbali, kushona charahani, na kusuka nywele, mwandishi ameyazungumza haya katika beti za (257 – 259, 262, 263,), mama yake alimfunza mtoto wake kazi hizi kwa lengo la kujipatia pesa ambazo zitamsaidia wakati atakapolewa. Katika beti za (265 na 266) msanii anasema,

265. *Kazi hizo hamfunza*

Tena nikamueleza

Haya ni yangu majaza

Nayatoa kifuwani .

266. *Haya utapolewa*

Kichwani utachukuwa

Pengine utachopewa

Hakikutoshi jikoni.

Vilevile Sihadaike aliusiwa kuacha maovu ambayo yatamletea madhara pindi atakapoyafanya (325 na 326), maovu hayo aliyokatazwa ni kama vile, kuacha hasada, kuacha fitna na fatani, kujiepusha na mkonomkono (wizi), kuacha zinaa na kuacha kunywa ulevi. Haya tunayapata katika *Utenzi wa Howani* beti za (327,331, 332, 333, 343, 346, 348, 349, 351, 353, 359, na 360). Sihadaike alikuwa ni mwari mtii, ambae aliyafuwata yote yale ambayo alifunzwa na wazazi wake, kiasi ambacho hakutoka nje hata siku moja na aliposikia watu wakibisha hodi nyumbani kwao, alijificha chumbani kwake ili asionekane. Msanii ameyazungumza haya katika beti za (32, 48 na 71) katika beti za (32 na 48) msanii anasema,

32. *Mwanamwali wa zamani*

Hatoki haonekani

Kila saa yumo ndani

Hasikiki abadani.

48. *Kukuwa kanyemelea*

Mlangoni kafikia

Kizingiti karukia

Kangia mwake chumbani.

Baada ya kuolewa Sihadaike alionekana na kizinda (bikira) na mumewe pamoja na wazazi wake walimtunza tunza mbalimbali. Tunza hizi alitunzwa kutokana na kujitunza na kujiheshimu kwake. Haya tunayapata katika beti za (636 -642, 790, - 794)

4.5.2.2 Mama yake Kukuwa

Mama yake Kukuwa ndie mtunzi wa tenzi hizi mbili. Mama huyu alizitunga tenzi hizi kwa lengo la kumueleza mtoto wake na jamii ya Kizanzibari kwa ujumla, mila na desturi ambazo walifanyiwa watoto wa kike hapo zamani,

kuanzia wanapozaliwa hadi kuolewa kama tunavyoona katika muhtasari wa kitabu hiki.

Beti za mwanzo katika utenzi wa *Howani*, mama yake Kukuwa ambae ndie mtunzi wa tenzi anaanza kwa kumpa mtoto wake historia kuanzia alipobeba ujauzito mpaka alipomzaa (6 -11). Mama huyu, ndie aliyemlea Kukuwa kwa mila na desturi zote ambazo mtoto anatakiwa kufanyiwa wakati wa kuzaliwa hadi atakapopewa mume au mke. Alimlea mtoto wake kwa kumfunza mambo yote mema kama vile dini na kupika (191, na 192), alimfunza kazi mbalimbali za amali (256), vilevile alimuusia mtoto wake kuacha mambo yote mabaya yasiyoridhiwa na Mwenyezi Mungu.

Ni yeye aliyemfunza mtoto wake jinsi ya kukaa na mume vizuri pamoja na wakwe zake pale alipoolewa na kupelekwa kwake, (1154 – 1172), katika beti za (1154 na 1155) msanii anasema,

1154. Yamemaliza ya somo

Anakuja mwana momo

Mama aliyekuwemo

Akingoja ukumbini .

1155. Wasia wake mrefu

Aloutunza kwa safu

Huo uliosadifu

Kumwasia mwafulani.

Mama huyu, alimuusia Kukuwa chungu ya mambo ambayo yatamsaidia kuishi vizuri na muumewe pamoja na wakwe zake pindi atakapoyafanya. Miongoni mwa mambo aliyomuusiya mwanawe ni: kumtunza mumewe, kufanya jambo analolipenda mumewe na kuacha jambo lolote analolichukia, kuwaheshimu

wakwe zake, kuendeleza kazi za amali alizomfunza ili amsaidie mumewe, kushika dini na kumuabudu Mwenyezi Mungu pamoja na kutekeleza nguzo tano za Kiislamu na nguzo sita za imani. Haya tunayapata katika beti za (1159, 1160, 1162 – 1171).

Mama Kukuwa, aliitumia nafasi yake vyema kwa kumlea mwanawe katika misingi ya mila na desturi zilizofuwatwa na jamii yake ya Kizanzibari hapo zamani, mila na desturi ambazo zilimlea mtoto katika maadili mema yenye kufuwata kiukamilifu dini ya Kiislamu ambayo siku zote humuongoza mwanadamu katika kufanya mema pindi anapoifuwata.

4.5.2.3 Bibi Mkunga

Bibi Mkunga, ni bibi ambae aliitwa na bibi yake Sihadaike kwa lengo la kwenda kumtazama mama yake Sihadaike maradhi yake, bibi huyu alimkanda mgonjwa na kubaini maradhi yake (15). Bibi Mkunga, alifanya kazi ya udaktari ya kuwapima na kuwazalisha wajawazito. Hii ni kwa sababu hapo zamani hapakuwa na madaktari wa kufanya hivyo (14 na 22). Ni yeye aliyemuanzisha mama Kukuwa mizungu ya kuilea mimba yake, wakati alipokuwa na ujauzito wa miezi sita kwa kumkanda kwa mafuta ya ufuta. Vilevile bibi huyu alimpokea mama Kukuwa wakati alipojifunguwa (55), na kumuimbia mtoto aliyezaliwa nyimbo mbalimbali za kumtakia makuzi mema na baadae akamkata kitovu mara tu baada ya kumpokea. Haya tunayapata katika beti za (56 – 58). Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki Bibi Mkunga ni ishara ya msimbo wa kiutamaduni, inayoashiria matabibu wa jadi ambao

hutumiwa na baadhi ya watu majumbani kwao, kuwapima na kuwapokea watoto wao wakati wa kujifunguwa, badala ya kuwapeleka hospitalini.

4.5.2.4 Bi. Mrashi

Huyu ni mpelelezi ambaye alitumwa na baba yake mumewe Kukuwa, kwa lengo la kwenda kufanya upelelezi nyumbani kwao Kukuwa kabla Kukuwa hajaolewa, (149) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*. Ni yeye aliyejigonga na dirisha na akaumia, wakati alipokwenda kupeleleza kwao akina Kukuwa lakini hakupiga kelele kwa vile kusudi haiambiwi pole, na hivyo Kukuwa hakumuona. Katika beti za (151 na 152) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa* msanii anasema,

151. Siku moja asubuhi

152. Kajigonga kaumiya

Kaja tafuta asahi

Walakini hakuliya

Lakini hakuiwahi

Anavyojuwa umbeya

Kajigonga dirishani.

Mrashi hawezekani.

Wakati wa kufanya upelelezi, Bi. Mrashi aliisikia sauti ya Kukuwa akimuhimiza mama yake kwenda kuswali (153). Baada ya kuisikia sauti ya Kukuwa na kuipenda, alikwenda kwa baba yake mwanamme anaetafutiwa mke kupeleka habari alizozipata kuhusu Kukuwa, haya tunayapata katika beti za (154, 161 – 164).

4.5.2.5 Somo Yake Kukuwa

Huyu ni muhusika ambaye alimuosha Kukuwa na kumpeleka kwenye unyago baada kuvunja ungo (9 na 10) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*. Somo ndiye

aliyemfundisha Kukuwa mambo mbalimbali yanayohusu maisha ya ndoa (16 - 20).

Mara baada ya baba yake Kukuwa kupokea posa za mtoto wake, bibi yake Kukuwa aliwashauri wanawe kumpelekea habari za posa somo yake Kukuwa kwa ajili ya kujitayarisha na kuja kupokea mahari. Beti za (369 na 370).

Bibi huyu ndie aliyekuwa mshuhulikiaji mkubwa wa Bi. Harusi kwa kumfanyia mambo mbalimbali (380), kama vile kusingwa na kupakwa hina (974 na 975). Vilevile, ni yeye aliyekaa kwa Bi. Harusi kwa muda wa wiki mbili, kwa lengo la kumuhimiza kuyatenda yote aliyomfunza alipokuwa mwari na aliyomfunza kuyafanya kabla hajapelekwa nyumbani kwake, beti za (1085 - 1087).

Mama huyu ndie aliyekwenda kukisafisha chumba cha Bi. Harusi na kukifukiza manukato kabla ya Kukuwa hajapelekwa kwake, ili akija yeye na mumewe wakikute chumba ni safi na kinanukia, (983 -985). Na mwisho bibi huyu aliitumia nafasi yake kwa kumfunza mwari wake jinsi ya kuishi vizuri na mume wake nyumbani kwake, (1105 – 1153). Somo anawakilisha watu ambao, hutumiwa na watu wengine katika familia, kuwafunda watoto wao mambo mbalimbali yanayohusu maisha kwa ujumla.

4.5.3 Matumizi ya Lugha

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) matumizi ya lugha katika utenzi ni ya kipekee yakilinganishwa na matumizi ya lugha katika bahari nyengine. Kwa

mfano, mtunzi wa utenzi ana uhuru mkubwa sana katika matumizi ya lugha, uteuzi wake wa msamiati, ubunifu wake, kubuni msamiati wake au maneno unde, kuyaendeleza maneno kwa njia tofauti. Katika kuchunguza matumizi ya lugha, tumechunguza kipengele cha tamathali za usemi ambazo ni tashibiha, tashihisi, sitiari na tafsida. Vilevile tumechunguza misemo na methali. Tumevichunguza vipengele hivyo kwa sababu vimetumika katika tenzi teule.

4.5.3.1 Tashibiha

Tamathali hii ya usemi hulinganisha vitu viwili ambavyo havihusiani, kwa kutumia maneno kama vile, kama, mithili, kwa mfano, sawasawa. Njogu na Chimera (2008). Mbinu hii inapotumika, msomaji au msikilizaji huweza kuchora taswira akilini mwake, jambo linalorahisisha kueleweka kwa kile kinachozungumzwa. Katika *Tenzi za Howani* na *Mwana Kukuwa* kuna baadhi ya matumizi ya tashibiha. Miongoni mwa tashibiha zilizojitokeza ni hizi zifuwatazo:

Tashibiha ya kwanza tunaipata katika ubeti wa (333) katika *Utenzi wa Howani*. Katika ubeti huo msanii anasema,

333. Fatani ni kama nyoka

Mwenye sumu isotoka

Ibilisi kumtaka

Kumtumia peponi.

Katika ubeti huo, fatani anafananishwa na nyoka kutokana na hatari aliyonayo. Katika hadithi na tenzi nyingi za Waswahili, muhusika nyoka, humithilishwa na muhusika mwenye hatari katika jamii ya Waswahili, kutokana na sumu kali aliyonayo. Hivyo kutokana na Nadharia ya Semiotiki fatani anarejelea mtu ambae ni hatari kwa sababu ya kufitinisha watu katika jamii, ambapo anafananishwa na sumu kali ya nyoka ambayo inaweza kumuuwa mwanadamu mara moja. Tashibiha nyengine imejitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*, katika ubeti wa (164) msanii anasema,

164. Sauti menipendeza

Kama njiwa anacheza

Tundu lake anaweza

Kuliranda kwa makini.

Katika ubeti huo sauti ya Kukuwa imefananishwa na sauti ya njiwa jinsi ilivyo nzuri. Kutokana na msimbo wa kiurejelezi, sauti ya Kukuwa inarejelea sauti ya mwanamke kigori ambae hajaolewa.

Vilevile kuna matumizi ya tashbiha katika ubeti wa (542), ambapo Bi. Mkali anafananishwa na pilipili kutokana na ukali alionao. Katika ubeti huo msanii anasema,

542. Bibi huyo, Bi Mkali

Kama vile pilipili

Bibi hanao muhali

Hana haya na imani

Katika tenzi hizi kuna matumizi makubwa ya tashibiha. Matumizi mengine ya tashibiha tunayapata katika beti (145, 146, na 173) katika *Utenzi wa Howani* na (76, 775, 1042, 1053, 1105, 1127, 1177) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*.

4.5.3.2 Tashihisi

Ni tamathali ya usemi ambapo viumbe visivyokuwa hai na vyenye uhai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna iliyo sawa na binaadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Aghlabu tamathali hii hutumiwa pia kurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za binaadamu. Dhima ya uhuwishi ni kutilia mkazo wazo au jambo fulani.

Tashihisi ni kipengele cha tamathali ya usemi kilichotumiwa na Bi. Zaynab Himid kwa lengo la kuibuwa mila na desturi mbalimbali katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika tenzi zake. Miongoni mwa tashihisi alizozitumia ni katika ubeti wa (646) katika *Utenzi wa Howani*, katika ubeti huo msanii anasema,

646. Furaha zachana nguo

Za mama wakati huo

Akasema kwa utuo

Twamshukuru Manani.

Tashihisi hii imetumika kwa ajili ya kuonesha jinsi mtu anavyokuwa na furaha za kupita kiasi, baada ya kupata jambo zuri. Mama Kukuwa, alikuwa na furaha nyingi kwa sababu ya mtoto wake kuonekana bikira. Kwa kawaida furaha zimepewa uwezo wa kuchana nguo kwa kurejelea furaha nyingi alizonazo mama mzazi baada ya mtoto wake kuonekana kizinda. Tashihisi nyengine imetumika katika ubeti wa (266) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa*. Msanii anasema,

266. Na bakora akashika

Bakora yatetemeka

Ya mpingo kadhalika

Kakamata mkononi.

Bakora imepewa uwezo wa kibinaadamu wa kutetemeka. Bakora hii ni bakora aliyoishika baba Kukuwa, wakati alipokwenda kupeleka habari za harusi kwa wazazi wake na mkewe. Hivyo bakora hii inarejelea msimbo wa kiutamaduni ambapo, wanaume wa visiwani hapo zamani pindi walipokuwa na safari walivaa kanzu, kofia, koti na walishikilia bakora kama utamaduni wao wa Kiislamu.

Vilevile kuna matumizi ya tashihisi katika ubeti wa (353) katika *Utenzi wa Howani*. Msanii anasema,

353. Fimbo hizo fimbi miya

Mojamoja kufwatiya

Hata vipi ukaliya

Zitalala mgongoni.

Kutokana na tashihisi hii msanii anarejelea msimbo wa kiutamaduni, pale ambapo mama Kukuwa anamtahadharisha mtoto wake na uzinifu. Bakora zimepewa uwezo wa kulala mgongoni kwa maana ya kupigwa kwa mtu aliyefanya tendo la zinaa kabla ya kuoa au kuolewa.

4.5.3.3 Tafsida

Hii ni tamathali ya usemi inayohusu kupunguza ukali wa maneno, kuna maneno ambayo hayakubaliki kutamkwa mbele ya jamii kama yalivyo yakimaanisha maana ya wazi. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) anasema kuwa tafsida ni mbinu ya kutumia maneno laini “yanayokubalika” mahali pa maneno “makali” yasiyokubalika kitamaduni au katika muktadha fulani kwa mfano “kwenda haja” badala ya “kukojowa”. Pia tafsida hutumika kuficha mawazo yenye hisia hasi au inayokera na hutumika katika mahusiano ya maneno yenye uwili. Reuson (1995).

Katika tenzi hizi msanii ametumia matumizi ya tafsida kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno. Katika ubeti wa (236) katika *Utenzi wa Howani* na ubeti wa (9) katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa* msanii ametaja tafsida ya “kuvunja ungo” badala ya “kutoka damu, au kuwa mwari”. Katika beti hizo msanii anasema,

236. *Pakambwa kuvunja ungo*

Kitaka kuwa na ringo

Asiambiwe msungo

Akatiwa uwarini.

9. *Kukuwa kavunja ungo*

Hampeleka kwa tungo

Kuchezwa siwe msungo

Aelewe mambo gani.

4.5.3.4 Sitiari

Katika ubeti wa (314) katika *Utenzi wa Howani* msanii ametumia sitiari kwa kulinganisha “majuto” na “mjukuu” bila ya kutumia viunganishi. Mwandishi ameitumia sitiari hii pale ambapo mama Kukuwa alipokuwa akimuusiya mwanawe juu ya kudumu na swala tano. Kwani asipofanya hivyo, atakwenda kujuta huko akhera na majuto yake hayatamsaidia chochote. Katika ubeti huo msanii anasema,

314. Majuto ni mjukuu

Mama wakati ni huu

Usali na kurukuu

Usingie mashakani.

4.5.3.5 Misemo na Methali

Misemo na Methali ni kunga za fasihi ambazo hutumia lugha ya mafumbo. Kunga hizi hutumika kupamba lugha na kufafanua maudhui. Methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kama kuwa kiwakilishi cha hekima na busara. Methali huwa ni sehemu ya turathi za jamii zinazobeba falsafa, mila, miiko, na desturi za jamii. Mbatiah (2001).

Misemo ni istilahi za fasihi ambazo huzaliwa, Kukuwa, na pengine hufa. Matumizi yake katika kazi ya fasihi sharti yategamee uhai wake katika matumizi yake ya kawaida katika jamii. Mwandishi wa tenzi hizi ametumia lugha ya mafumbo katika methali na misemo kufafanuwa mila na desturi mbalimbali za mwanamke zilizojitokeza katika tenzi hizo. Miongoni mwa

methali na misemo iliyotumiwa na mwandishi imejitokeza katika beti zifuwatazo.

42. *Haya mpaji ni Mungu*

Kusubiri kilimwengu

Tutapata letu fungu

Haitofika mwakani.

Msemo huu ulitumiwa na mamaake Kukuwa katika *Utenzi wa Mwana Kukuwa* baada ya Kukuwa kuvunja ungo na kurudi unyagoni, kipindi ambacho Kukuwa yuko nyumbani na anasubiri mume. Mama huyu aliosema msemo huu “haya mpaji Mungu” kwa kumaanisha kwamba Mungu ndie anaetowa riziki za waja wake, hivyo na yeye hatochoka kusubiri hadi mtoto wake atakapopata fungu lake litokalo kwa Mwenyezi Mungu (yaani muume).

Katika ubeti wa (330) *Utenzi wa Howani* mama yake Sihadaike alitumia msemo wa “Mola hamwachi mjawe” pale alipokuwa akimuusia mwanawe juu kukinai na anachokipata na kushukuru na asichokipata, kwani Mola hamwachi mjawe. Methali na misemo mengine imejitokeza katika beti zifuwatazo : (930, 1052, 1216, 1223) n.k.

4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili data tulizozikusanya katika tenzi teule. Data zimechambuliwa kwa kutegemea malengo mahsusi ya utafiti pamoja na mpangilio wa maswali ya utafiti huu. Sura inayofuwata imejadili muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatowa muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Sura hii imegawika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu tumetoa mapendekezo kwa wasomi na watafiti wa siku za usoni.

5.2 Muhtasari

Katika utafiti huu, tulikusudia kuchunguza na kutathmini mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazojidhihirisha katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*. Utafiti huu una malengo mahsusi matatu ambayo ni: kuainisha mila na desturi zinazojitokeza katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*, kuchambuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazopatikana katika tenzi teule na kubainisha mbinu za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi teule.

Utafiti ulikusudia kujibu maswali yafuwatayo: Je, ni mila na desturi zipi zinazojitokeza katika tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa*? Ni mila na desturi gani katika usawiri wa mwanamke wa visiواني zinazopatikana katika tenzi teule? Je, ni mbinu zipi za kifani zilizotumika kuibuwa mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiواني katika tenzi husika?

Utafiti huu ulikuwa ni wa maktabani, ambao data zake zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Sosholojia na Nadharia ya Semiotiki katika kuyachambua malengo yake mahsusi matatu. Utafiti huu una umuhimu wa kuelezea mila na desturi za wanawake wa visiwani wa hapo zamani, jinsi walivyozitekeleza na kuzienzi mila na desturi zao. Matokeo ya utafiti huu ni kama yafuwatayo:

Utafiti huu umebaini kuwa, wanawake wa visiwani hapo zamani, walikuwa wakizithamini mila na desturi zao kwa kuzitekeleza katika nyanja mbalimbali za maisha. Mila na desturi ambazo walikuwa wakizitekeleza zilijitokeza katika vipengele vifuwatavyo: malezi ya mimba na wakati wa kujifunguwa, katika malezi ya watoto, elimu, sherehe za unyago, mafunzo au kufunda, ngoma za asili, tiba za asili, ndoa, mapambo ya asili pamoja na mavazi.

Tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* zinaonekana na upekee kwa kiasi fulani. Hii ni kutokana na ukweli ya kuwa, tenzi hizo zimejadili kwa kiasi kikubwa mila na desturi za mwanamke wa visiwani kuanzia alipozaliwa hadi alipopelekwa kwake kwa kufungishwa ndoa. Mara tu mtoto alipozaliwa alifanyiwa mila na desturi mbalimbali ambazo walizirithi kutoka kwa mabibi zao. Mila hizo ni: kulelewa kwa madawa mbalimbali, kulazwa kwenye ungo wenye mchanga, kufanya sherehe za kutoa jina kwa mtoto, kupelekwa chuoni n.k.

Tenzi hizi zimeonesha kuwa, miongoni mwa mila na desturi ya wanawake wa visiwani waliyoifanya kwa watoto wao wa kike ni kuwapeleka unyagoni pale

walipovunja ungu. Huko walifunzwa mafunzo mbalimbali yanayohusu usafi na maisha ya ndoa. Vilevile wanawake hawa, waliwafunza watoto wao mambo mbalimbali yanayohusu dini yao ya Kiislamu, kama vile nguzo za Kiislamu na nguzo za imani. Pia waliwakataza mambo ambayo yamekatazwa katika dini yao kama vile, kunywa ulevi, kuiba, kuzini n.k. Pia waliwafunza kazi za amali ambazo ziliwasaidia kupata pesa wanapokuwa kwa waume zao na kuwasaidia . Miongoni mwa kazi walizofunzwa ni: kusuka ukili, kushona makawa, miteka na miswala, kushona charahani, kusuka nywele n.k.

Pia mwandishi wa tenzi hizi amezungumzia kwa kiasi kikubwa mila na desturi katika kipengele cha ndoa, ambapo ndoa ilikuwa ni makubaliano baina ya wazazi wa mtoto wa kike na mtoto wa kiume. Wazazi wa mtoto mwanamme walipomtafutia mtoto wao mke, waliwatumia wapelelezi kwa ajili ya kuwachunguza wari majumbani mwao. Endapo tabia za mtoto mwari zikikubalika wazee hawa hupeleka posa. Na wazazi wa mtoto wa kike walizichunguza tabia za watu walioleta posa, wakiridhika nazo hupokea mahari na kufungisha ndoa.

Katika tenzi hizi wanawake wa visiwani walitumia madawa mbalimbali ya asili ambayo yalitumika kama kinga na tiba kwa ajili ya kuondoa husda na maradhi. Miongoni mwa dawa hizo ni: mvuje, habasoda, majani ya mbono na nyingi nyenginezo. Katika kipengele cha elimu wanawake hawa hawakuwapeleka watoto wao shuleni kwa kukhofia kupotoka. Mtoto wa kike alipewa elimu ya dini kwa kupelekwa Madrasa, na alifunzwa mambo mbalimbali na mama yake yanayohusiana na dini yao.

Kwa upande wa mavazi, wanawake hawa walivaa mavazi kwa kufuwata mila na desturi zao. Mavazi waliyovaa ni kama vile: mabaibui yenye vizoro, kanga mbili, kanga za kisutu kwa ajili ya Bi. Harusi, kanzu, mitandio, vilemba, ukaya, kigwe n.k. Vilevile wanawake hawa walitumia mapambo na manukato kwa ajili ya kujipamba na kunukia vizuri mwilini mwao na katika majumba yao.

Mapambo hayo yalitumiwa wakati wa sherehe mbalimbali kama vile sherehe za harusi, wakati wa matembezi, na hata wakati wa kuwastarehesha waume zao. Miongoni mwa mapambo na manukato yaliyotumiwa na wanawake hawa ni: asumini na vilua, manargisi, mihanuni, mawardi, udi na ambari, hal-udi, vikuba, dalia, utunda, marashi, tunda za marijani, hina, wanja n.k. Vilevile walivaa bangili, vidani, vipini na vikuku, vitu hivyo vilikua vya dhahabu, fedha au kareti.

Pia wanawake wa visiwani walikuwa na vyama mbalimbali vya kupiga na kucheza ngoma. Vyama hivyo vilikodiwa katika sherehe tofauti kwa ajili ya kutoa burudani. Miongoni mwa ngoma zilizopigwa na vyama hivyo ni: lele mama, bomu, tarabu, beni, msondo, na hata maulidi ya Mtume (S.A.W) ambayo yalisomwa kwenye harusi.

Mbinu za kifani zilizotumika kuibua mila na desturi katika tenzi hizi ni mandhari, wahusika na lugha. Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa data tulizozikusanya, tuligunduwa yafuwatayo yanahusiana na fani ya tenzi hizi.

Kwanza tumegunduwa kuwa tenzi hizi zimetumia mandhari ya Upwa wa Afrika Mashariki kwa mfano, mandhari yaliyotumika ni mandhari ya visiwa vya Unguja na Pemba; kwa vile mila na desturi alizozieleza mtunzi zinawahusu watu wanaoishi katika visiwa hivyo.

Kuhusu wahusika, tenzi za *Howani* na *Mwana Kukuwa* zimetumia wahusika wa kawaida na wahusika wa kiutamaduni. Wahusika wa kawaida ni kama vile: Mama yake Kukuwa, ambae ndie aliyemfanyia mtoto wake mila na desturi zilizokuwemo katika jamii yake wakati huo, Babaake Kukuwa, Muumewe Kukuwa, Babaake Muumewe Kukuwa, ambao nao kwa kiasi kikubwa walisaidia kueleza utamaduni wa jamii iliyokusudiwa.

Wahusika wa kiutamaduni waliotumiwa ni Mshenga (mposaji), Bi. Mrashi (mpelelezi), Bi. Mkunga ambae alimpokea Kukuwa wakati alipozaliwa na Somo ambae ndie aliyempeleka unyagoni Kukuwa na kumshughulikia katika harusi yake kuanzia kupokea mahari hadi alipopelekwa kwake.

Katika kipengele cha lugha tumegunduwa kuwa, msanii ametumia Kiswahili cha Unguja na baadhi ya vitongoji vyake, ambacho kinazungumzwa na watu wa visiwa hivyo viwili. Vilevile katika tenzi hizi kuna matumizi makubwa ya tashibiha, tashihisi, sitiari tafsida pamoja na misemo na methali. Bi. Zaynab Himid Mohammed amevitumia vipengele hivyo kwa ufundi wa hali ya juu, kwa lengo la kuhakikisha kwamba tenzi zake zinakuwa na mvuto kwa wasikilizaji na wasomaji wake, pamoja na kufikisha ujumbe alioukusudia katika jamii yake.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchambua data zinazohusiana na mila na desturi katika usawiri wa mwanamke wa visiwani katika *Tenzi za Howani* na *Mwana Kukuwa*. Mila na desturi za mwanamke wa visiwani zilionekana hazijafanyiwa utafiti katika tenzi husika. Hivyo hali hii ilimpelekea mtafiti kuona ipo haja ya kufanya utafiti katika kipengele hiki ili kupunguza pengo la kitaaluma. Matokeo ya utafiti wetu yameonesha kuwa, mila na desturi za mwanamke wa visiwani zimeelezwa vizuri na mtunzi na zimetupatia mwanga wa kuweza kuzichambuwa na kuziwasilisha kwa urahisi.

Juhudi za mwandishi, kutunga tenzi hizi, zimefanikiwa vizuri katika kushughulikia mila na desturi za mwanamke wa visiwani. Katika uchanganuzi huo imebainika kwamba, tenzi hizi zimesheheni mila na desturi wanazozifanya wanawake wa visiwani kuwafanyia watoto wao, kuanzia wanapowazaa hadi kuwafungisha ndoa na kuwapeleka kwa waume zao. Mila hizo zimejitokeza katika vipengele vifuwatavyo: malezi ya mimba na kujifunguwa, malezi ya watoto, elimu, tiba, mavazi, ngoma, sherehe za unyago, pamoja na ndoa.

Kupitia kwa wahusika tofauti waliotumiwa na mwandishi, msomaji anaweza kujifunza mambo kadhaa wa kadhaa ambayo ni mila na desturi za wanawake husika. Kwa mfano, kupitia muhusika Somo, ni dhahiri kuwa msomaji ataelewa baadhi ya mila na desturi kutokana na uhusika wake aliobebeshwa kwa Kukuwa. Muhusika huyu alimfanyia Somo yake mambo mbalimbali ambayo ni mila na desturi zao. Miongoni mwa mambo aliyomfanyia mwari wake (Kukuwa) ni: kumpeleka unyagoni, kumsinga, kumpaka hina, kumremba

na kumpamba kwa mapambo mbalimbali wakati alipoolewa, kumpeleka kwa muumewe n.k.

Kwa hivyo, ni dhahiri ya kwamba Bi. Zaynab Himid Mohammed amefaulu katika lengo lake la kuelimisha wasomaji kuhusu mila na desturi zao walizozifanya hapo kale kwa watoto wao wa kike, kupitia katika tenzi zake za *Howani* na *Mwana Kukuwa*.

5.4 Mapendekezo

Diwani hii ya *Howani Mwana Howani*, imefanyiwa utafiti kadhaa wa kadhaa lakini bado sehemu nyingi ambazo kwa sababu ya wakati na mada tuliyoifanyia utafiti haikuwezekana kuzijadili zote.

Utafiti huu umeshughulikia mila na desturi katika fasihi andishi, kwa kurejelea *Tenzi za Howani* na *Mwana Kukuwa*. Hata hivyo hatuwezi kusema kwamba utafiti huu umekamilika na kwamba *Tenzi za Howani* na *Mwana Kukuwa* haziwezi kufanyiwa uchunguzi mwingine wowote. Mapendekezo yetu ni kwamba vipengele vyengine vya utamaduni kama vile: itikadi, miko, silka na vyenginevyo, vifanyiwe uchambuzi ili kubainisha ikiwa vinaweza kuwasilishwa kwa kutumia nadharia ya Sosholojia.

Tenzi hizi pia, zinaweza kufanyiwa utafiti kwa kutumia Nadharia nyengine tofauti na zilizotumika, kama vile Nadharia za Ufeministi, Ufeministi wa Kiislamu na Nadharia ya Umuundo kwa ajili ya vipengele vya fani, ili wasomaji waweze kudurusu yaliyomo kutokana na mitazamo mengine tofauti.

Kuna haja ya watafiti wa baadae, kushughulikia vipengele vya fani ambavyo hatujavishughulikia, kama vile mtindo, muundo na baadhi ya vipengele vya lugha alivyovitumia mwandishi kama uendelezaji wa mila na desturi katika tenzi husika. Sisi tumeshughulikia wahusika, mandhari na matumizi ya lugha.

Mwisho tunapendekeza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Elimu, ijumuishe somo la mila na desturi za Kizanzibari katika mtaala wa elimu kuanzia shule za msingi hadi Vyuo Vikuu.

MAREJELEO

- Abeid, R. S. na Olutu, S. R. (2009). *Civics for Secondary School*. Dar es Salaam: Oxford University Press Tanzania Ltd.
- Ali, (2015). *Nafasi ya Mwanamke wa Kipemba Kama Inavyosawiriwa Katika Hadithi Simulizi za Waswahili Pemba*:Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Alhidaya [Http://w.w.w. alhidaya.com/sw/node/1305](http://w.w.w. alhidaya.com/sw/node/1305).
- Al- kindy, S. M. M. (1988). *Mkweli Muaminifu. Katika Mafunzo ya Bwana Mtume (S.A.W). Juzuu ya Kwanza na ya Pili*. Oman: Muscat Bookshop Sultanate of Oman.
- Babie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bakhresa, S. K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- BAKIZA, (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar: Quark Xpress Printing Services.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd
- Barthes, R. (1968). *Element of Semiology*. New York: Hill and Wang.
- Brunitti, I. (2005): *Ngoma ni Uhunu? Ngoma za Kisasa Mjini Zanzibar*. Swahili: Forum12(205):161-17katika<http://www.qucosa.de/fileadmini/data/qucosa/documets/9770/12-12-Brunotti>.

- Creswell, J. (2009). *Quantitative, Qualitative, and Mixed Method Approach*. London: SAGE Publication.
- Dezidery, K (2010). *Uchambuzi wa Utenzi wa Mwanakupona : Mawaidha katika Tendi*. File:///c:/users/USER/documents/mwanakupona.htm/.
- El- maawy, A. A. A. (2011). *Jawabu la Mwanakupona. Mausiyo ya Mke wa Kisasa na Wasia wa Mwanakupona*. Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Emmanuel, F. (2015). *Wakaazi wa Pwani ya Afrika Mshariki Wanavyodumisha Utamaduni wa Mswahili*. [Http://archieive.habarileo.co.tz/index.php/makala/38395](http://archieive.habarileo.co.tz/index.php/makala/38395).
- Enon, J. C. (1998). Education Research, Statistics and Measurement. *Educational psychology Journal*, 2(4) 70 – 83..
- Faki, (2015). Sifa za Kifani za Utendi Mfano :Utendi wa Fumo Liongo: Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Huria cha Tanzani. Dar es Salaam, Tanzania.
- Gatakaa, (2012): “Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa. Tasnufu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Hamad, O. (2014). Kuchunguza Mabadiliko na Maendeleo ya Kasida Visiwani Zanzibar Baada ya Mapinduzi na Wakati wa Soko Huria : Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.
- Harton, M. na Middleton, J. (2000). *The Swahili the Social Landscape of a Mercantile Society*. New York: Backwell Publishers Ink.
- Hornsby, A. (2000). *Advanced Learner's Dictionary 6th ed*. London: Oxford University Press.

- Hucker, K. (2001). *Research Methods in Health. Care and Early Years*. London: Heinmann Educational Pub.
- Hussein, V. (2014). Uchunguzi Kuhusu Mchango wa nYimbo na Simulizi za Matambikokatika Kurithisha Mafunzo, Mila, na Desturi za Wakaguru wa Mamboya. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
- Juma, K. B. (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar: Quark Xpress Printing Services.
- Kahigi, K. K. (1994). *Lugha katika Vitabu vya Watoto Katika Kioo cha Lugha: Jarida la Kiswahili Isimu na Fasihi*. Dar es Salaam: Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Juzuu Na. 1. (uk: 21-36).
- Kamati ya Tamasha ya Utamaduni wa Jamii ya Wairaqw na Wagorowa Wilaya ya Babati. *Historia na Chimbuko, Mila na Desturi za Kabila la Wagorowa*. [Http://www.safarilands](http://www.safarilands).
- Khatib, M. S. (1985). *Utenzi wa Mwanakupona katika Mulika NA. 17*. Dar es Salaam: taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu.
- Kileo, S. E. (2011). Nafasi ya Mudhui ya Filamu za Kiswahili katika Kuakisi Maswali ya Kijamii. Uhakiki wa Filamu za Taswira na Vita vya Ushindi. Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Kivenule, A. (2013). Mila na Tamaduni za Kabila la Wahehe katika Mkowa wa Iringa : [Http://www.adamkivenule blogs](http://www.adamkivenule blogs).
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (p) Ltd.

- Low, N. R. (2011). *Athari ya Lugha katika Kuibuwa Dhamira : Mifano Kutoka katika Nyimbo za Kizazi Kipya Zihusuzo UKIMWI*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.
- Massamba, D.P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbatiah, M. (2011). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mbayi, L. A. (2009). *Uhakiki wa Fani katika Tenzi za Howani na Mwanakukua*. Tasnifu ya M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mdee, na wenzake, (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*, Dar es Salaam: Longhorn Pubishers.
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religion and Philosophy*. London: Heinman.
- Mdungi, A. (2000). *Dhana ya Utenzi wa Mapokeo. Zanzibar: Ministry of Education katika Jarida la Elimu Zanzibar Toleo Na 1 : 30-37. Zanzibar, Tanzania.*
- Mercey, (2011). Mtazamo wa Mhari na Utamaduni. Katika [Http://harusinamaendeleo.wordpress.com\(2011/11/11/10/mtazamo-wa-mahari-na-utamaduni/](http://harusinamaendeleo.wordpress.com(2011/11/11/10/mtazamo-wa-mahari-na-utamaduni/)
- Mohammed, Z. H. (2004). *Howani Mwana Howani*. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: DUP.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers Ltd.

- Mulokozi M. na Kahigi, K. K. (1997). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Hria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mwinyi, A. H. (2004). *Howani Mwana Howani*. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Ngonyani, Y. (2010). *Mila na Desturi za Wangoni Upande wa Ndoa na Kuchumbia*. File /// G:// Mila na Desturi za Wasomi. Html.
- Njau, M. na wenzake (2013). *Sheria ya Ndoa na Talaka*. Katika [Http://womenslegalaidcentre.org/file/Sheria ya Ndoa na Talaka BOOK .pdf](http://womenslegalaidcentre.org/file/Sheria%20ya%20Ndoa%20na%20Talaka%20BOOK.pdf).
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nurse, D. and Spear, T. (1985). *The Kiswahili Reconstruction The History and Language on a African Society 800-1500*. Philadelphia :University of Pennsylvania Press.
- Omar, C. K. (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu. Mtaala ya Lugha na Fasihi* Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Omar, C. K. (1997). *Misemo na Methali Toka Tanzania. Kitabu cha Kwanza*. Arusha: Arusha Eastern Africa Publications.
- Otoro, (2012). Msimbo wa Maana katika Tamthiliya ya Zilizala: Tasnifu ya M. A.Chuo Kikuu cha Nairobi. Kenya

- Pauline, R. (2013). Uhakiki wa Maudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemuozea: Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Kenya.
- Ponera, A. S. (2014). Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Dodoma: Karljamier Print Technology.
- Rawson, H. (1995). *Euphemism Definition, Synonyms from Answers*. Com katika W.W.W. Answers. Com/topic/euphemism. Iliyosomwa 19/02/2012.
- Sameja, M. A. (2002). *Twahara Swala na Mambo Yanayomukhusu Maiti*. IQRA: Zanzibar.
- Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature*. New Delhi: Yale University Press.
- Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es salaam: AERA Kiswahili Researched Products.
- Sengo, T. S. Y. (1991). *Itikadi katika Jamii za Waswahili, katika Mlacha*, S. A. K. na Kurskieri, (1995), *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Sengo, T. S. Y. (1985). *The Indian Ocean Complex and The Kiswahili Fotklore: The case of Zanzibar Tel-performance*. Phd Khartoum University, Sudan.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Simon, (2014). *Ishara katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo : Mtazamo wa Kisemiotiki* : Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairbi. Kenya.
- Swaleh, A. (2004): “*Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupo*”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Kenya.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai Industries Ltd.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misngi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Kenya Lithotho Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publication.